

**CHANGAMOTO ZA UTOHOAJI WA MANENO YA KIINGEREZA
KATIKA KISWAHILI**

MTORO MCHUKIVU BAKARI

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA, IKIWA NI SEHEMU YA MASHARTI YA
KUTUNUKIWA SHAHADA YA UZAMILI (M.A. KISWAHILI ISIMU)
KATIKA IDARA YA LUGHA NA TAALUMA ZA FASIHI YA
CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

2022

UTHIBITISHO

Aliyeweka saini hapa chini anathibitisha kwamba amesoma tasnifu hii ya utafiti yenye anuani “*Changamoto za Utohoaji wa Maneno ya Kiingereza Katika Kiswahili*” kwa ajili ya kukamilisha masharti ya shahada ya MA. Kiswahili (Isimu) katika idara ya Lugha na Taaluma za Fasihi ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Dkt. Salma Othmani Hamad

(Msimamizi)

Tarehe _____

HAKI MILIKI

Hairuhusiwi kukaririwa au kuhawilishwa kwa mbinu ya kielektroniki kama kunakili, kutoa kopi au kurudufu sehemu yoyote ya tasnifui hii bila ya idhini kutoka kwa mwandishi wa tasnifu hii au Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa niaba yake.

TAMKO

Mimi **Mtoro Mchukivu Bakari** ninatamka na kuthibitisha kwamba tasnifu hii ya utafiti inayohusu “*Changamoto za Utohoaji wa Maneno ya Kiingereza Katika Kiswahili*” ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kutolewa popote pale kwa lengo la kutunukiwa shahada yoyote katika Chuo Kikuu chochoto.

Sahihi _____

Tarehe _____

TABARUKU

Ninaitabaruku tasnifu hii kwa mama yangu mzazi Bi. **Mwajabu Jumu** kwa kunipigania ili nijiendeleze katika masomo yangu, na hatimaye kujitegemea kiuchumi.

SHUKURANI

Matokeo na mafanikio ya kazi hii yametokana na michango na mawazo ya watu na taasisi mbalimbali. Kwa hakika si rahisi vikundi vyote kuvitaja au kutaja majina yao kwa kila aliyehusika. Hata hivyo, nalazimika kuwataja wachache walioshiriki kwa namna moja ama nyingine kufanikisha utafiti huu. Awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai na afya njema iliyonisaidia kuifanya kazi hii kwa wepesi.

Pili, namshukuru msimamizi wangu Dkt. Salma Hamad kwa juhudi zake kubwa za kuniongoza katika mchakato huu na kunifanya niione kazi hii ni nyepesi japo ilikuwa ngumu. Alinivumilia katika madhaifu mbalimbali yaliyokuwa yakijitokeza kwangu kama mwanadamu na mwanafunzi wake alisimama upande wangu ili niweze kuifanya kazi hii vizuri. Kila wakati hakuchoka kunishauri na kuniongoza katika kuhakikisha namaliza kazi hii kwa muda uliopangwa, Mungu ambariki sana na ampe moyo wa subira.

Tatu, napenda kuishukru familia yangu kwa kuwa karibu na mimi katika kipindi chote cha uandishi wa tasnifu hii. Namshukuru mke wangu kipenzi Malkia Salim, mtoto wangu Nadir M. Bakari na kaka yangu Ally Bakari.

Nne, naushukuru uongozi na wafanyakazi wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Makao makuu kwa kunipa fursa ya kufanya utafiti kwa muda muafaka na katika eneo ambalo nililopendekeza kufanyia utafiti. Pia nawashukuru kwa kunipangia msimamizi mzuri Dkt. Salma O. Hamad, bila kuwasahau wahudumu wa maktaba ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa jinsi walivyoweza kunisaidia kwa kunipatia kila maandiko na vitabu ambavyo vilikuwa vinaendana na kazi yangu ya utafiti.

Ushirikiano huo ulinifanya kukamilisha kazi hii kwa wakati hasa kipindi cha kuandika pendekezo la mswada na wakati wa uchambuzi wa data.

Tano, napenda kuwashukru Wakurugenzi wa taasisi zinazohusika na ukuzaji lugha ya Kiswahili nchini Tanzania za BAKITA na TATAKI kwa kunipatia kibali cha kufanya utafiti katika ofisi zao. Barua zao za utambulisho kwa wafanyakazi wao zilinipatia upenyo mkubwa sana wa kupata ushirikiano kutoka kwa wafanyakazi hao. Vilevile, ninawashukuru wafanyakazi wa BAKITA na TATAKI kwa ushirikiano wao walionipa katika ukusanyaji wa data za utafiti huu. Mawazo yao ndiyo yaliyowezesha kukamilisha kazi hii kwa wakati.

Sita, nawashukuru wanafunzi wenzangu wote wa M.A Kiswahili (Isimu, 2017/2019) kwa ushirikiano wao walionipa wakati wote wa masomo yetu hususan katika mijadala mbalimbali ya kitaaluma iliyokuwa inaibuka darasani. Mijadala hiyo ilinipa mwanga wa kuanza kuyaona mambo kwa mtazamo tofauti katika mijadala hiyo imenipatia chachu katika uandishi wa tasnifu hii.

IKISIRI

Tasnifu hii ilikuwa na lengo kuu la kuchunguza changamoto za utohoaji wa maneno ya Lugha ya Kiingereza katika lugha ya Kiswahili nchini Tanzania. Katika kufikia lengo kuu hilo, malengo mahususi matatu yamehusishwa ambayo ni kubainisha mbinu za utohoaji wa maneno ya Kiingereza katika lugha ya Kiswahili, pili, kuelezea athari za utohoaji wa maneno ya Kiingereza katika lugha ya Kiswahili na tatu, kufafanua changamoto za utohoaji wa lugha ya Kiingereza kwenye lugha ya Kiswahili. Utafiti huu ulifanyika katika taasisi za umma zinazojihusisha na ukuzaji wa lugha ya Kiswahili nchini Tanzania ambazo ni BAKITA na TATAKI ambazo zote zipo mkoani Dar es Salaam. Njia zilizotumika kuwapata watoa taarifa ni usampulishaji nasibu na usi nasibu. Usampulishaji nasibu ulitumika kwa wasimamizi wakuu wa idara. Usampulishaji usio nasibu ulitumika kwa wafanyakazi wa idara. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Mkabala wa Mlingano Chanzi ulioasisiwa na Smith, mwaka 2006. Nadharia hii imechaguliwa na mtafiti kwani ina uwezo unaoruhusu mikakati mbalimbali urekebishaji wa maneno yaliyotoholewa. Katika ukusanyaji wa data kutoka katika eneo la utafiti, mtafiti alitumia njia ya mahojiano na dodoso. Jumla ya watafitiwa waliohusika katika utafiti huu walikuwa ni 43. Utafiti huu umebaini kuwa utohoaji wa maneno hutokana na kuibuka kwa dhana mpya katika jamii za kilimwengu kutokana na ukuaji wa kimaendeleo.

Maneno Makuu: *Kutohoa, mlingano chanzi, Kiswahili, Kiingereza*

YALIYOMO

UTHIBITISHO	ii
HAKI MILIKI.....	iii
TAMKO.....	iv
TABARUKU	v
SHUKURANI.....	vi
IKISIRI.	viii
YALIYOMO.....	ix
ORODHA YA MAJEDWALI.....	xiii
ORODHA YA VIFUPISHO.....	xiv
SURA YA KWANZA: UTANGULIZI	1
1.1 Usuli wa Mada	1
1.2 Tatizo la Utafiti	6
1.3 Malengo ya Utafiti	7
1.3.1 Lengo Kuu	7
1.3.2 Malengo Mahsusi.....	7
1.4 Maswali ya Utafiti.....	7
1.5 Umuhimu wa Utafiti	8
1.6 Vikwazo vya Utafiti	9
1.7 Mipaka ya Utafiti	10
1.8 Mpangilio wa Utafiti.....	11
SURA YA PILI: MAPITIO YA KAZI TANGULIZI	12
2.1 Utangulizi.....	12

2.2	Makutano ya Lugha	12
2.3	Utohoaji wa Maneno Kutoka Lugha Moja Kwenda Lugha Nyingine	15
2.4	Pengo la Maarifa	17
2.5	Nadharia ya Utafiti.....	17
2.5.1	Nadharia ya Mlingano Chanzi	18
2.6	Hitimisho.....	21

SURA YA TATU: MBINU ZA UTAFITI

3.1	Utangulizi.....	22
3.2	Eneo la Utafiti	22
3.3	Usampulishaji	22
3.3.1	Usampulishaji Nasibu	23
3.3.2	Usampulishaji Usio Nasibu.....	23
3.4	Sampuli	24
3.5	Mchanganuo wa Wahojiwa.....	25
3.6	Mbinu za Kukusanyia Data.....	25
3.6.1	Mbinu ya Mahojiano	25
3.6.2	Mbinu ya Dodoso.....	26
3.7	Mbinu za Kuchanganua Data.....	27
3.8	Udhabiti wa Data	28
3.8.1	Kuaminika kwa Data.....	29
3.9	Hitimisho.....	29

SURA YA NNE: UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA

4.1	Utangulizi.....	31
-----	-----------------	----

4.2	Mbinu za Utohoaji wa Maneno ya Kiingereza katika Lugha ya Kiswahili .	31
4.2.1	Utohoaji wa Moja kwa Moja na Mabadiliko ya Matamshi	31
4.2.2	Utohoaji wa Moja kwa Moja Bila Mabadiliko	34
4.2.3	Udondoshwaji wa Irabu Katikati ya neno.....	36
4.2.4	Uingizaji wa Irabu Mwishoni mwa Neno	37
4.2.5	Uingizaji wa Irabu Katikati ya Neno	39
4.2.6	Udondoshaji wa konsonanti katika Konsonanti kikundi	40
4.3	Athari za Utohoaji wa Maneno ya Kiingereza katika Lugha ya Kiswahili .	42
4.3.1	Ukuzaji wa Msamiati wa Lugha ya Kiswahili	42
4.3.1.1	Upande wa Afya	42
4.3.1.2	Upande wa Elimu.....	43
4.3.1.3	Upande wa Biashara	43
4.3.2	Mfuatano wa Sauti Unaokubalika Katika Lugha ya Kiswahili.....	44
4.4	Changamoto za Utohoaji wa Maneno ya Kiingereza katika lugha ya Kiswahili.....	45
4.4.1	Kudumaza Lugha	45
4.4.2	Ukiukwaji wa Kanuni ya Mkazo Katika Utamkwaji wa Maneno ya Lugha ya Kiswahili.....	46
4.4.3	Changamoto ya Mfuatano wa Sauti Isiyo Katika Muundo wa Lugha ya Kiswahili	47
4.4.4	Kasumba ya Wazungumzaji wa Lugha ya Kiingereza	48
4.4.5	Upungufu au Ufinyu wa Mbinu za Utohoaji	49

SURA YA TANO: MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO	50
5.1 Utangulizi.....	50
5.2 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti	50
5.3 Hitimisho.....	52
5.4 Mapendekezo ya Utafiti	53
MAREJELEO	54
VIAMBATISHO	59

ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali 3.1:	Sampuli Iliyokusudiwa	25
Jedwali 4.1:	Utohoaji wa Moja kwa Moja na Mabadiliko ya Matamshi	32
Jedwali 4.2:	Utohoajiwa Moja kwa Moja bila Mabadiliko	35
Jedwali 4.3:	Udondoshaji wa Irabu katikati ya neno.....	37
Jedwali 4.4:	Uingizaji wa Irabu Mwishoni mwa Neno	38
Jedwali 4.5:	Uingizaji wa Irabu katikati ya neno	40
Jedwali 4.6	Udondoshaji wa Konsonanti katika Konsonanti Kikundi.....	41
Jedwali 4.7:	Mfuatano wa Sauti Unaokubalika Katika Lugha ya Kiswahili.....	44
Jedwali 4.8:	Changamoto ya Mfuatano wa Sauti isiyo Katika Muundo wa Lugha ya Kiswahili	48

ORODHA YA VIFUPISHO

BAKITA	:	Baraza la Kiswahili la Taifa
TATAKI	:	Taasisi ya Taaluma ya Kiswahili
TUKI	:	Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

1.1 Usuli wa Mada

Kwa mujibu wa uchunguzi uliofanywa na Guthrie (1962), Kiswahili kiliwekwa katika kundi la lugha za Kibantu na kwamba kulikuwa na ishara za kuzungumzwa kwa lugha hii kwenye maeneo ya Pwani ya Afrika Mashariki kabla ya karne ya kumi. Polome (1967: 9) anaeleza neno “Kiswahili” lina asili yake katika neno la Kiarabu “sawahil” (kwa wingi “sahil”) lenye maana ya “pwani”. Wazungumzaji wa Kiswahili nao wakarejelewa kama “Waswahili”.

Polome (1967) anafafanua kuwa, pamoja na maeneo ya Afrika Mashariki, Kiswahili pia kinazungumzwa katika janibu za Afrika ya Kati, Afrika Kusini, eneo la Kusini mwa Oman kule Uajemi. Pia anazidi kufafanua maingiliano baina ya Waswahili na wageni kutoka nchi zingine ambapo anadai kuwa rekodi za kihistoria kama vile tarihi za Kilwa zinaonyesha maingiliano baina yao na wageni. Maingiliano hayo yanaibuka katika miktadha ya dini, biashara, ndoa, utawala na mengineyo. Baadaye ukoloni ulipokita mizizi kwenye maeneo haya ya Afrika Mashariki katika karne ya kumi na tisa, Kiswahili kilitekeleza wajibu muhimu kwani kilitumika katika kufanikisha shughuli za kikoloni hasa zile za kiutawala, isitoshe pia kilitumika kutekeleza majukumu ya kielimu.

Lugha ya Kiswahili ina historia ndefu ya kuingiliana na lugha tofauti. Mwingiliano huo wa lugha umeiathiri lugha ya Kiswahili kwa kuingizia maneno mabalimbali yaliyotoholewa. Kwa ufafanuzi wa Thomason (1976: 165) utohoaji wa maneno ni dhana ya kiisimu inayoelezea uchukuaji neno au elementi yoyote kutoka lugha moja

kwenda katika lugha nyingine. Naye Massamba (1989: 64) anasema utohoaji ni uhamishaji wa istilahi kutoka lugha moja kwenda lugha nyingine. Wanafafanua kwamba aghalabu maneno yanayokopwa ni maneno ya kiufundi, kwa maana ya maneno ya taaluma, inaweza kuwa ni ya sayansi na teknolojia au taaluma yoyote ile.

Massamba, (ameshatajwa) anasema kuwa katika karne ya 19, Afrika Mashariki iliingia kwenye uhusiano na mataifa mengine kama vile Ujerumani na Uingereza. Uhusiano huo ni baada ya watu wa pwani kuwa na uhusiano wa muda mrefu wa kibiashara na Waarabu. Waarabu walipoingia waliweka athari kubwa katika kukua na kuenea kwa lugha ya Kiswahili. Wageni kutoka Ulaya walipoingia Afrika Mashariki walifanya biashara, shughuli za kidini elimu na utawala. Kama ilivyokuwa katika kipindi cha Wareno na Waarabu kuwepo kwao pia kulikuwa na athari katika maendeleo ya lugha ya Kiswahili Afrika Mashariki na kwingineko.

Utawala wa Wareno: Wareno walivamia na kutawala pwani ya Afrika Mashariki baina ya miaka ya 1505 hadi 1698 B.K. Utawala wao ulikuwa wa kikatili uliohusisha uporaji na uharibifu mkubwa sana wa miji ya pwani ya Afrika Mashariki. Juhudi za wenyeji wa pwani kupambana na vikosi vya Kireno vilivyotumia silaha bora ikilinganishwa na zao duni, hazikufua dafu. Shariff Noor (1988:4) akiwanukuu wanahistoria Coupland na Basil Davidson anatuelezea kuwa miji kama vile Mombasa na Faza ilihujumiwa vikali zaidi. Wareno hawakuteka nyara tu bali waliuwaua wanaume, wanawake, watoto, hata mbwa waliofugwa majumbani pamoja na makasuku pia vidau, mashua na ngarawa zilizokuwa bandarini zilichomwa moto. Milima ya ngawira ilikusanywa- dhahabu, fedha, pembe za ndovu, ambali, ng'ombe, na vyakula vingine. Ngawira ilikuwa kubwa mno, hata ikabidi mali nyingine iachwe,

kwani hakukuwa na nafasi katika meli zao. Hivyo basi, Wareno waliweza kuingiliana na Waswahili katika muktadha wa kiutawala, na kibiashara ambapo umeweza kuleta athari ya maneno katika lugha ya Kiswahili kama vile; karata na matunda, Nanasi, kamba, vifaa, meza, bendera, na gwaride.

Kipindi cha Waarabu: Massamba (2010) anasema kuwa, Waarabu walifika katika pwani ya Afrika Mashariki mnamo karne ya 18. Walipofika wakakuta wenyeji wakizungumza lugha zao za Kibantu kikiwemo Kiswahili. Waarabu hasa katika pwani ya Afrika Mashariki walifanya biashara, ikiwemo biashara ya watumwa, ambayo ilikuwapo na misafara mbalimbali ya biashara kutoka pwani hadi bara. Katika misafara hiyo, Kiswahili ndiyo iliyokuwa lugha ya mawasiliano hivyo Kiswahili kikaenea pia katika sehemu za bara. Kuna mambo kadhaa waliyofanya Waarabu ambayo yalichangia kukua kwa lugha ya Kiswahili. Waarabu walichangia kukua kwa lugha ya Kiswahili kama ifuatavyo;

Biashara: Waarabu walifanya biashara kati ya pwani na sehemu za bara, katika biashara yao walichangia uenezaji wa lugha ya Kiswahili. Lugha kuu ya mawasiliano na ya kibiashara iliyotumiwa na wafanyabiashara wa Kiarabu ilikuwa ni Kiswahili. Kwa njia hii waliweza kueneza Kiswahili kuanzia pwani hadi maeneo ya bara kama vile Morogoro, Dodoma, Tabora, Kigoma hadi Mashariki mwa Kongo.

Dini: Dini ilichangia uenezaji wa lugha ya Kiswahili kupitia mawaidha na mafunzo ya madrasa. Waarabu walipokuja walitaka kueneza dini ya Kiislamu katika maeneo waliyofikia. Hivyo, walianzisha madrasa ambayo walitumia kufundisha huku wakitumia lugha ya Kiswahili.

Maandishi ya Kiarabu: Waarabu pia walileta hati zao zilizotumiwa katika maandishi ya lugha ya Kiswahili. Kwa hiyo kupitia hati za Kiarabu maandishi mbalimbali ya lugha ya Kiswahili yaliweza kuhifadhiwa. Hivyo Kiswahili kilikua kutokana na kuhifadhiwa katika maandishi na kusomwa wakati wowote.

Kwa ujumla, tunaweza kusema kuwa ujio wa Waarabu umeiathiri lugha ya Kiswahili. Kwa mujibu wa Zawawi (1979) athari ya lugha ya Kiarabu katika msamiati wa lugha ya Kiswahili ni kubwa. Kufuatana na uchunguzi wa Zawawi (1979) maneno 3,006 yaliyoorodheshwa katika kamusi ya *Johnson's Standard Dictionary* maneno 2,354 ni mkopo kutoka katika lugha ya Kiarabu. Athari ya lugha ya Kiarabu katika Kiswahili iliendelea kutokana na kuwepo kwa Waraabu katika pwani ya Afrika Mashariki na biashara yautumwa.

Kipindi cha Wajerumani: Kwa mujibu wa Massamba (2010) Wajerumani waliingia pwani ya Afrika Mashariki mwaka 1875. Wajerumani walipowasili nchini Tanzania walitumia Kijerumani kwa mawasiliano yao katika utawala na elimu. Wajerumani walikipiga vita Kiswahili kwa kuogopa mfungamano wake na Uislamu na pia uwezo wa kuwaunganisha pamoja wananchi wazalendo. Hali hii ilidumaza maendeleo ya Kiswahili nchini. Katika elimu Wajerumani walifungua shule za serikali zilizotumia lugha ya Kijerumani hata baada ya kuruhusu matumizi ya Kiswahili kutumiwa katika elimu. Kiswahili kilitumika tu kufundishia elimu ya msingi na kukwamisha maendeleo yao hasa kwa elimu ya juu. Wajerumani walidharau lugha ya Kiswahili na kuiona lugha duni ikilinganishwa na lugha ya Kijerumani. Hivyo hata mwingiliano wao haukuweza kuiathiri sana lugha ya Kiswahili kama utawala wa mataifa mengine. Aidha, kuja kwa Wajerumani katika karne ya 19 BK kulisababisha Kiswahili

kuathiriwa na Kijerumani kwa kupata maneno yalitokana na Kijerumani ni kama shule, (schule) na hela (heller) Massamba (2010).

Kipindi cha Waingereza: Thomason na Kaufman (1988:19) wanaeleza kuwa muathiriano unakuwa wa kiwango kikubwa kadri lugha zinavyodumu pamoja na kwa muda mrefu. Athari za lugha ya Kiingereza na Kiarabu katika Kiswahili ni za kiwango kikubwa ikilinganishwa na lugha nyingine kwa sababu ya maingiliano ya muda mrefu baina ya Waswahili na Waingereza na Waarabu.

Lugha ya Kiingereza ilipata nafasi ya kukiathiri Kiswahili kwa sababu ya utawala wa muda mrefu wa wakoloni wa Kiingereza, kutokana na jinsi utawala wa kikoloni ulivyoipa nafasi lugha hiyo ya Kiingereza kutumika hasa katika shughuli za utawala. Waingereza baada ya kuchukua utawala wa Tanganyika kutoka kwa Wajerumani miaka ya 1930, waliendelea kutumia Kiswahili kama lugha ya utawala hadi wakaamua kukisanifisha ili kiweze kukidhi haja ya mawasiliano katika makoloni yao ya Afrika Mashariki. Usanifishaji wa lugha ya Kiswahili ulisimamiwa na Kamati ya Kiswahili ya Afrika Mashariki iliyojulikana kama “Interterritorial Language Committee”. Madhumuni makuu ya kusanifisha lugha ya Kiswahili yalikuwa kuhakikisha kwamba kuna aina moja ya msamiati wa zamani ulioazimwa katika kamusi zote, hasa kamusi za shule na kusahihisha na kusanifisha lugha ya vitabu vyote vilivyopendekezwa kutumiwa shuleni (Mbaabu, 2007:27).

Hata baada ya wakoloni wa Kiingereza kuondoka wakati Tanganyika ilipopata uhuru wake mwaka 1961, Kiingereza kiliendelea kutumika sanjari na lugha ya Kiswahili. Ijapokuwa Kiswahili kilishatambuliwa kuwa ni lugha ya Taifa na lugha rasmi mwaka 1962 lugha ya Kiingereza ilipewa nafasi ya kutumika katika nyanja muhimu. Leo hii

Kiingereza ni lugha rasmi ikisaidiana na lugha ya Kiswahili ikiwa lugha rasmi, pia Lugha ya Kiingereza inaendelea kutumika katika mawasiliano yanayohusu masuala ya nje, kufundishia elimu ya juu, uandishi katika baadhi ya magazeti, na mahakama za ngazi ya juu na kadhalika. Hivyo, Kiingereza kinaendelea kuiathiri lugha ya Kiswahili hadi leo. Athari ya lugha ya Kiingereza katika Kiswahili inaonekana zaidi katika utohoaji wa maneno.

Kwa mujibu wa Batibo (2000:240) lugha ya Kiingereza imetumika katika kuendeleza lugha ya Kiswahili kutokana na hadhi yake kama lugha ya sayansi, elimu na teknolojia katika kukuza maendeleo ya kiuchumi, kisayansi, kielimu na kijamii. Ili maneno hayo yanayotoholewa yaweze kuwa sehemu ya lugha ya Kiswahili inabidi yaingizwe katika muundo wa lugha ya Kiswahili ili yakubalike kuwa sehemu ya msamiati wa lugha hiyo. Kwa hiyo, utafiti huu umechunguza changamoto za utohoaji wa maneno ya lugha ya Kiingereza katika Kiswahili.

1.2 Tatizo la Utafiti

Utaratibu wa kutohoa maneno kutoka lugha moja na kuyatumia kwenye lugha nyingine hutokea kwa lugha zote duniani. Utohoaji wa maneno ya lugha moja na kuyatumia katika lugha nyingine huchangiwa na sababu mbalimbali kama vile teknolojia ambayo huwa inakuja na maneno mapya ambao lugha nyingine haina. Mapitio ya kazi mbalimbali za utafiti yanaonesha kuwa lugha ya Kiswahili imetohoa baadhi ya maneno kutoka katika lugha mbalimbali ikiwemo lugha ya Kiingereza. Watafiti kama Kenstowizs na Suchato (2006), wamejadili namna ambavyo lugha mbalimbali zimekuwa zikitohoa maneno kutoka katika lugha nyingine. Hata hivyo, tafiti zao hazikugusia changamoto zinazojitokeza katika mchakato wa utohoaji wa

maneno kutoka lugha moja kwenda lugha nyingine, kutokana na mwiingiliano huo. Lugha ya Kiswahili imetohoa maneno kutoka katika Lugha ya Kiingereza, ambapo tafiti nyingi zimejikita katika kuonesha namna maneno yanavyotoholewa, lakini kwa namna moja ama nyingine utohoaji huo umekua na changamoto kwa namna moja ama nyengine, Katika utafiti huu mtafiti amejikita katika kujadili changamoto za utohoaji wa maneno ya Kiingereza katika lugha ya Kiswahili.

1.3 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu una lengo kuu na malengo mahususi ambayo ni kama yafuatayo:-

1.3.1 Lengo Kuu

Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza changamoto za utohoaji wa maneno ya lugha ya Kiingereza katika lugha ya Kiswahili.

1.3.2 Malengo Mahususi

Malengo mahususi ni haya yafuatayo:

- i. Kubainisha mbinu za utohoaji wa maneno ya Kiingereza katika lugha ya Kiswahili.
- ii. Kueleza athari za utohoaji wa maneno ya Kiingereza katika lugha ya Kiswahili.
- iii. Kufafanua changamoto za utohoaji wa maneno kutoka katika lugha ya Kiingereza kwenda lugha ya Kiswahili.

1.4 Maswali ya Utafiti

- i. Ni mbinu zipi hutumika katika utohoaji wa maneno ya Kiingereza katika lugha ya Kiswahili?

- ii. Kuna athari zipi za utohoaji wa maneno ya Kiingereza katika lugha ya Kiswahili?
- iii. Ni changamoto zipi hujitokeza wakati wa utohoaji wa maneno ya Kiingereza katika Kiswahili?

1.5 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu, unalenga kuonesha changamoto ya utohoaji wa maneno ya Kiingereza katika lugha ya Kiswahili, hivyo basi utafiti huu umelenga kufanikisha harakati za kuelewa muundo wa ndani wa lugha pokezi. Manufaa yake ni kuwa wanaisimu watazidi kuelewa sarufi za lugha za kiasili za Kiafrika huku ikizingatiwa kuwa, lugha hizi hazijapewa nafasi kubwa katika mifumo ya elimu ikilinganishwa na lugha za kigeni. Hii inatokana na wazo kwamba uamilifu wa baadhi ya kanuni za kifonolojia na kimofolojia za lugha hudhihirika wazi zaidi kanuni zenyewe zinapotumika kugeuza maneno ili yaweze kuingia katika mfumo wa lugha-pokezi. Kwa hivyo, uchunguzi huu utapanua uelewa wa kanuni mbalimbali za kifonolojia na kimofolojia za lugha ya Kiswahili.

Pia, utafiti huu utawafaidisha walimu wa lugha ya Kiingereza kwani wanaweza kuutumia kuelewa matatizo yanayoweza kuwakabili wanafunzi wanaojifunza lugha ya Kiingereza; hasa matatizo yale yanayotokana na lugha ya kwanza. Haya ni matatizo yanayotokana na mtagusano baina ya lugha yao ya kwanza (Kiswahili) na lugha ya Kiingereza.

Hali kadhalika, uelewa wa mchakato wa utohozi ni muhimu kwa kuwa unadhihirisha namna ambavyo maneno mapya huingia katika lugha mahususi. Kutokana na umuhimu wa suala hili, wataalamu wamejaribu kuchanganua lugha kwa madhumuni

ya kupata ufahamu wa kina kuhusu utaratibu wa utohozi. Hivyo basi, utafiti huu unaongeza maarifa kwenye harakati hizi za kutaka kuelewa mchakato mzima wa utohozi hasa katika muktadha wa lugha za Kiafrika. Maarifa ya aina hiyo yatawafaa watafiti na wasomi wa baadaye ambao wangependa kufahamu mengi zaidi kuhusu utohozi hasa kutoka katika lugha ya Kiingereza kwenda katika lugha ya Kiswahili.

Zaidi ni kuwa, watu wanaojifunza lugha ya Kiswahili kwa mara ya kwanza pia wanaweza kufaidika kutokana na utafiti huu. Sababu ni kwamba, wataweza kutumia data zilikazotokana na utafiti huu kurekebisha makosa ya kifonolojia na kimofolojia ambayo yanaweza kutokea katika harakati zao za kujifunza lugha ya Kiswahili. Isitoshe, wanaofanya tafsiri na ukalimani (kutoka lugha zingine kwenda Kiswahili) pia wataweza kunufaika kutokana na uchunguzi huu kwani utohozi ni mojawapo ya mikakati inayoweza kutumiwa katika taratibu za tafsiri au ukalimani. Hivyo wanaoweza kufaidika kwa namna hii ni kama vile wataalamu wanaotafsiri kutoka lugha ya Kiingereza kuelekea lugha ya Kiswahili. Kwingineko watumiaji wa Kiswahili katika kazi zingine kama vile utangazaji kwenye redio na uana-habari kwa ujumla nao wanaweza kubaini utaratibu mwafaka wa kutohoa maneno mageni yanayoingia katika lugha ya Kiswahili.

1.6 Vikwazo vya Utafiti

Katika kazi ya utafiti, mtafiti alikumbana na vikwazo kama ugumu wa kuwapata watoa taarifa kutoka baraza la Kiswahili(BAKITA) na taasisi inayojihusisha na taaluma ya Kiswahili (TATAKI), ambao ndio wahusika wakuu katika zoezi la utohoaji. Mara nyingi walikuwa na kazi zingine za kitaifa miongoni mwazo ni kusimamia masomo ya vitendo, kusahihisha mitihani ya wanafunzi wa chuo kikuu

cha Dar Es Salaam pamoja na kuwa na vikao mbalimbali vya kiutendaji vya mara kwa mara, ingawa baadaye mtafiti alifanikiwa kuwafikia na kukusanya data kutoka kwao kwa kuwapigia simu mara kwa mara ili kjuua ratiba zao za vikao za kiutendaji, kutumia muda mwingi kwenda katika eneo la utafiti, hii ni kutokana na kila mmoja alikua na ratiba yake ya kiutendaji kwa wakati huo.

Pia kuchelewa kupata data kwa wakati tuliokubaliana kwa njia ya dodoso kutokana na dharura zilizo nje ya uwezo wa watafitiwa na hasa ni kushughulishwa na majukumu yao ya kiutendaji.

Vile vile kuchelewa kujibiwa kupewa kibali kitakahoniruhusu kukusanyia data kutoka katika taasisi inayojishughulisha na taaluma ya Kiswahili (TATAKI), hii ni kutokana na mkuu wa idara kuwa na safari ya kikazi, na hatimaye ilichukua muda kidogo kujibiwa kwa wakati.

1.7 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu ulijikita zaidi katika kuchunguza changamoto za utohoaji wa maneno ya lugha ya Kiingereza katika Kiswahili. Mtafiti alifanyia utafiti wake Taasisi ya Taaluma za Kiswahili (TATAKI) katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA). Mtafiti alitumia malengo matatu tu ambayo yako katika tasnifu hii, ambayo ni kubainisha mbinu za utohoaji wa maneno ya Kiingereza katika lugha ya Kiswahili, kuelezea athari za utohoaji wa maneno ya Kiingereza katika lugha ya Kiswahili, na kufafanua changamoto za utohoaji wa misamiati kutoka katika lugha ya Kiingereza.

1.8 Mpangilio wa Utafiti

Utafiti huu una jumla ya sura tano. Sura ya kwanza ambayo ina utangulizi, ndani yake kuna utangulizi wa mada ya utafiti, tatizo la utafiti, lengo kuu la utafiti, malengo mahususi ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, vikwazo vya utafiti, na mipaka ya utafiti. Sura ya pili ni mapitio ya kazi tangulizi ambayo ndani yake kuna vipengele vya utangulizi, kazi tangulizi, nadharia za utafiti na hitimisho. Sura ya tatu ni njia za utafiti, ambayo inahusu mbinu za kukusanyia data, mbinu za kuchanganua data na udhibiti wa data. Sura ya nne inahusu uchanganuzi wa data, ambao unahusu malengo makuu matatu ya utafiti ambayo yamechanganuliwa na kuchambuliwa kwa kina, kisha kutoa hitimisho. Sura ya tano ni muhtasari, matokeo, na mapendekezo ya maeneo ambayo watafiti wengine wanaweza kujikita katika kufanya utafiti.

SURA YA PILI

MAPITIO YA KAZI TANGULIZI

2.1 Utangulizi

Sura hii ina sehemu kuu mbili. Sehemu ya kwanza ni ya kazi tangulizi. Katika sehemu hii kazi za tafiti mbalimbali zinazohusiana na makutano na kuathiriana kwa lugha pamoja na utohoaji wa maneno zimejadiliwa. Sehemu ya pili imefafanua kwa kina nadharia iliyotumika katika utafiti huu.

2.2 Makutano ya Lugha

Thomason (2001) anafafanua dhana ya makutano ya lugha kuwa ni matumizi ya lugha zaidi ya moja katika sehemu hiyo hiyo na katika wakati huo huo. Maingiliano ya lugha yalikuwepo miaka mingi, ingawa taaluma hii ya mwingiliano wa lugha ilianza kushamiri karne ya 18. Suala hili limekuwa kivutio kwa watafiti wa historia ya lugha walipotambua ukweli kwamba hakuna lugha inayoweza kuwa nje na sifa ngeni (pasipokuwa na athari na lugha nyingine). Miongoni mwa mambo yanayotajwa kuwa ni sababu za makutano ya lugha hususani kwa miaka ya hivi karibuni ni hamahama ya watu wa jamii lugha katika jamii lugha nyingine, wanajamii wa lugha tofauti kuwa katika ujirani wa muda mrefu, kuoana na elimu (makutano wakati wa ujifunzaji).

Thomason (2001) anatoa mifano ya makutano ya jamii za Wabantu Wakoisani. Matokeo ya makutano hayo, Kikoisani kiliathiri Kibantu hasa Kizulu ambacho kilijipatia sauti bainifu ya kidoko. Aidha, katika utafiti wake Thomason 2001 (ameshatajwa) uliochunguza makutano ya lugha za Kindendeule, Kimatengo na Kingoni, Ngonyani (1989) amebaini kuwa Kingoni kimeathiriwa na lugha hizo mbili.

Kingoni hakikuwa na fonimu /l/ lakini kutokana na athari za lugha hizo ambazo zimeizunguka lugha ya Kingoni, kwa sasa Kingoni kinayo fonimu hiyo. Naye Haule (2014) ameonesha athari za kiisimu za Kiswahili katika lugha ya Kingoni kama vile vitenzi *nitiweza* kutokana na *tunaweza*, *tikoroma* kutokana na *tunakoroma*, *lokota* kutokana na *okota*, *atolwiki* kutokana na *alitoroka*, *wolewa* kutokana na *olewa*, *shangala* kutokana na *shangaa*, *mshonai* kutokana na *shoneni*.

Tafiti za Thomason (2001), Ngonyani (1989) na Haule (2014) zinabainisha kwamba, lugha zinapoathiriana zinaweza kubadilishana sauti, maumbo au miundo ya maneno hasa kama sauti, maumbo au miundo Fulani ambayo hua haipo katika lugha moja. Hivyo, lugha inayoathiriwa huanza kutumia sauti, maumbo au miundo ambayo awali haikuwa miongoni mwa vijenzi vya lugha inayohusika. Maelezo haya yanathibitishwa na Sankoff (2001) anapoeleza kuwa matokeo ya kiisimu kutokana na makutano ya muda mrefu ya lugha zaidi ya moja ni kuweza kupotea kwa sifa za vipashio, kuwa na vipashio vya ziada pamoja na kubadilishana vipashio miongoni mwa lugha hizo. Vilevile, tafiti hizi zinatudhihirishia kwamba, awali athari za makutano ya lugha ziliangaliwa zaidi katika uga wa isimu. Hata hivyo, kwa sasa Agyekum (2006) anasema maendeleo ya taaluma ya makutano ya lugha kiisimu yamebadilika kwa kuifanya kuwa changamani mno ambapo hata masuala ya sosholojia, anthropolojia, ethnolojia na saikolojia yanahusishwa. Tunaelezwa pia kuwa, mtazamo wa kiisimujamii katika mwingiliano wa kiisimu ulileta mwanga kwa masuala mengi ndani ya mawanda ya tafiti zinazohusu mwingiliano au ukopwaji/utohoaji wa kiisimu.

Katika suala la utohoaji, Mbaabu (2007) ameeleza athari ya makutano ya Waarabu na Waswahili kwa muda mrefu katika mwambao wa Afrika Mashariki. Miongoni mwa

athari hizo ni Kiswahili kuchukua maneno ya kidini na ya vifaa vya kigeni vilivyoletwa kutoka nje. Baadhi ya maneno ya Kiswahili yalitokana na athari ya lugha ya Kiarabu ni *wakil* kuwa *wakili*, *rahim* kuwa *rehema*, *salaam* kuwa *salama*, *shukran* kuwa *shukurani*, na mengineyo. Wareno nao walikiathiri Kiswahili kwa kuingiza maneno kama *mezr* kuwa *meza*, *benjera* kuwa *bendera*. Aidha, Haule na Katunka (2012) wanatoa mifano ya maneno ya Kiswahili ambayo ni athari ya lugha ya Kiingereza kama vile *sweater* kuwa *sweta*, *history* kuwa *historia*, *shirt* kuwa *shati* na *lesso* kuwa *leso*.

Kwa ujumla, tunaweza kusema kwamba pale ambapo jamii lugha mbili zinakutana kila lugha huathiri au kuathiriwa na lugha nyingine katika kiwango kimoja cha kiisimu ama kingine. Hivyo, kuathiriana kwa lugha ni tabia ya kawaida miongoni mwa lugha za ulimwengu. Ingawa aghalabu lugha zenye nguvu ndizo zinazoziathiri zaidi lugha zisizo na nguvu, bado uwezekano wa lugha zisizo na nguvu kuathiri lugha zenye nguvu upo. Mfano mzuri uliobainishwa na Mbunda (2002) ni neno *Ikulu* kutoka katika lugha ya Kinyamwezi, *ng'atuka* kutokana na lugha ya Kizanaki na *ngeli* kutoka katika lugha ya Kihaya.

Maandiko haya kwa ujumla yametubainishia kuwa kila lugha zaidi ya moja zinapokutana ni lazima zitaathiriana. Miongoni mwa athari zinazopatikana ni utohoaji wa maneno kutoka lugha moja kwenda katika lugha nyingine. Hata hivyo, hakuna maelezo yoyote yaliyotolewa kuhusu changamoto zinazojitokeza katika mchakato huo wa utohoaji wa maneno. Suala hili ndilo lililochunguzwa katika utafit huu.

2.3 Utohoaji wa Maneno Kutoka Lugha Moja Kwenda Lugha Nyingine

Owino (2003) anafafanua kuwa, maneno ya mkopo huweza kutambuliwa kupitia utaratibu wa kulinganisha leksimu za lugha lengwa na zile za lugha changizi. Katika utafiti huu, ulinganishaji huu ulitegemea vigezo kama vile makaribiano ya kisemantiki kati ya dhana mbalimbali, mfanano wa kifonimu kati ya leksimu pamoja na mkondo wa utohoaji kati ya lugha husika. Hali kadhalika, Iribemwangi (2013) anatambua kuwa iwapo kuna utohoaji wa leksimu kutokana na mtagusano baina ya lugha, aghalabu pia kuna uwezekano wa kukopa vipengele vya kitamaduni vinavyohusishwa na lugha zenyewe. Harakati hizi zitaongozwa na ujuzi wa mtafiti wa lugha zinazotafitiwa. Dhana ya utohoaji maneno imeelezwa na Crystal (1987) kama mkakati wa kuingiza neno au vipengele vingine vya kiisimu katika lugha maalum, aghalabu vipengele kama hivi hutokana na lugha au lahaja zingine. Maneno ambayo yanaingia katika lugha fulani kwa njia hii ndiyo hurejelewa kama maneno-mkopo. Utohoaji wa maneno hutokana na mtagusano baina ya lugha tofauti (Arlotto, 1972) na ndio unaobadilisha maneno katika vikoa mbalimbali vya kisemantiki. Kwa hivyo, utohoaji maneno hujaza pengo fulani la kimaana katika lugha pokezi. Baadhi ya nyanja zenye maneno ya mkopo ni pamoja na elimu, upishi, uchukuzi, biashara, ukulima, vyombo vya nyumbani na utawala.

Iribemwangi na Mukhwana (2011:156) wanaeleza kwamba, utohoaji wa maneno hutokana na kuibuka kwa dhana mpya katika jamii za kilimwengu kutokana na ukuaji wa kimaendeleo. Hii ni kumaanisha kuwa lugha sharti iwe na mikakati teule ambayo ilitumika ili kubuni msamiati mpya wa kurejelea dhana kama hizo. Njia mojawapo ya kuunda maneno mapya ni kutohoa.

Sambamba na hayo, Kenstowizs na Suchato (2006) wanatambua kwamba utohozi wa msamiati unahusisha marekebisho yanayoongozwa na masharti. Wanashikilia kwamba, katika hali halisi kwenye mchakato wa kutohoa maneno, mzungumzaji huwa na nia ya kudumisha uaminifu kwa lugha changizi na wakati huo, kufanya maneno-mkopo kuwa na ruwaza ya vipande-sauti na sifa arudhi ambazo zinakubalika katika lugha pokezi. Uaminifu unaorejelewa hapa ni uhifadhi wa sifa za kifonolojia zinazojitokeza katika lugha changizi; yaani sifa hizi zijitokeze katika lugha pokezi kadri inavyowezekana.

Kwa upande mwingine, Karuru (2012) anachunguza utohozi wa kifonolojia na kimofolojia wa maneno-mkopo ya Gi-Gichugu (lahaja ya Gikuyu) ambayo yanatokana na Kingereza na Kiswahili kwa kutumia Mkabala wa Mlingano Chanzi. Uchunguzi huu unadhihirisha kwamba Gi-Gichugu hutumia michakato anuwai katika kutohoa maneno-mkopo kutoka lugha ya Kiswahili na Kingereza. Michakato hiyo ni pamoja na uambishaji, udondoshaji, uchopekaji na nyinginezo. Hata hivyo, maneno yaliyokopwa hujitahidi kufanana kifonolojia na maneno ya lugha changizi.

Lehman (1975) kwa upande wake anafafanua namna ambavyo utohoaji-maneno huweza kuathiri mifumo ya kifonolojia ya lugha pokezi. Anasema kuwa utohoaji-maneno katika lugha ya Kingereza (kutokana na lugha ya Kifaransa na Kirusi) umeathiri ruwaza ya kifonolojia ya Kingereza kwa vile sauti geni zimeweza kuingizwa katika lugha ya Kingereza. Sauti hizo ni pamoja na /dʒ/ na /sk/ ambazo kiasilia si sauti za lugha ya Kingereza.

Pamoja na tafiti hizo, tafiti nyengine ambazo pia zinagusia utohozi wa maneno-utohoaji ni Mbonankira (2004) ambaye anashughulikia utohozi wa msamiati wa

Kiswahili na Kingereza kuingia lugha ya Kinyarwanda na Kimani (2005) anayeangazia utohozi wa msamiati-mkopo kutoka lugha ya Gikuyu kuingia lugha ya Kimasai. Tafiti hizo zimefafanua mageuzi ya kifonolojia, kimofolojia na hata ya kisemantiki ambayo neno huyapitia ili liweze kukubaliana na mifumo ya lugha pokezi. Hata hivyo, tafiti zao hazijatoa maelezo kuhusu changamoto zinazojitokeza wakati mchakato huo wa ubadilishaji wa maneno unapofanyika. Utafiti huu umechunguza changamoto zinazojitokeza wakati maneno mkopo ya Kiingereza yanapogeuzwa ili yakubaliane na kanuni za kifonolojia na za kimofolojia za lugha ya Kiswahili.

2.4 Pengo la Maarifa

Baada ya kusoma kazi mbalimbali za tafiti tangulizi zinazohusu utohozi katika lugha, mtafiti amegundua kuwa kazi hizo zimejikita zaidi kuangalia msamiati wa uliotoholewa katika lugha, pamoja na mabadiliko ya msamiati huo kifonolojia, kimofolojia na hata kisemantiki. Kazi hizo hazikuchunguza changamoto za utohozi na hivyo kuonekana kuwa utohoazi ni mbinu salama ambayo mtu yeyote anaweza kufanya kwa namna anavyoona yeye ni sahihi. Utafiti huu umezionesha changamoto za utohoaji wa maneno ya Kiingereza katika Kiswahili.

2.5 Nadharia ya Utafiti

Nadharia ni mawazo, maelezo au mwongozo uliopangwa ili kusaidia kueleza, kutatua au kutekeleza jambo fulani (TUKI, 2013). Katika utafiti, nadharia ni muongozo ambao mtafiti anaufuata ili kutekeleza kwa ufanisi utafiti wake. Massamba (2004) anasema kuwa, nadharia ni taratibu kanuni na misingi ambayo imejengwa katika miundo ya kimawazo kwa madhumuni ya kutumiwa kama kielelezo cha kueleza

jambo. Kwa mantiki hiyo nadharia ni dira na mwongozo wa kulikabili jambo kifalsafa, kidini, kimantiki, kijamii na kiutamaduni. Katika utafiti huu, mtafiti amejadili nadharia ya mkabala wa Mlingano chanzi.

2.5.1 Nadharia ya Mlingano Chanzi

Utafiti huu umeongozwa na nadharia ya Mlingano Chanzi (Smith, 2006) ambayo inatokana na mihimili ya Nadharia ya umbo Upeo. Nadharia ya umbo Upeo yenyewe iliasisiwa na Prince & Smolensky, (1993). Nadharia ya Umbo Upeo haikuanza kama nadharia iliyoshughulikia utohozi wa maneno. Nadharia hii ilianza kuchanganua masuala ya kifonolojia katika lugha. Uchughuzi wa mabadiliko ya lugha umeanza katika miaka ya 1995 na kuendelea.

Nadharia ya Mlingano Chanzi inaruhusu mikakati mbalimbali ya kiutohozi ambayo inatokana na uelewa wa mtohoaji pamoja na fasiri za kifonolojia. Hali kadhalika, mkabala huu unasisitiza kanuni ya uaminifu baina ya umbo-fikirika la lugha changizi, ambayo kwa mujibu wa utafiti wetu ni lugha ya Kiingereza, na umbo- tamkwa katika lugha pokezi ambayo kwa mujibu wa utafiti wetu ni lugha ya Kiswahili. Kwa hivyo, mtafiti aligundua kuwa kuna ulinganifu kati ya umbo-fikirika la lugha changizi kutoka katika lugha ya Kiingereza na umbo la neno lililotoholewa.

Kwa hivyo, inasisitizwa kwamba vipengele vya umbo la lugha changizi sharti vijitokeze katika umbo la lugha pokezi. Kwa upande wa pili, vipengele vyote katika umbo la neno katika lugha pokezi sharti vijitokeze katika umbo la neno la lugha changizi. Hata hivyo, Mkabala wa Mlingano Chanzi bado unaruhusu mikakati ya urekebishaji wa maneno yaliyotoholewa. Umbo fikirika la lugha changizi unajengeka kutokana na ujuzi wa tahajia wa lugha hiyo, uelewa wa sarufi ya lugha changizi,

pamoja na fikra alizonazo mtohoaji kuhusu lugha changizi. Umbo hili fikirika si lazima lifanane na umbo la neno linalotokana na lugha changizi (ambalo ndilo hutoholewa). Kwa mfano, msamiati wa lugha changizi (Kiingereza) “Wiper” kwenye lugha pokezi (Kiswahili) linakuwa “Wepa”.

Omary na Richards (1966) wanasema kuwa, umbo fikirika la msamiati wa lugha changizi hufanyiwa marekebisho anuwai ili uweze kufuata masharti ya kifonolojia na mofolojia ya lugha pokezi. Kwa mfano, mkakati wa udondoshaji wa irabu na uchopekaji wa irabu katika mbinu za utohaji wa maneno ya Kiingereza katika lugha Kiswahili, unaweza kutumiwa ili kuondoa vipande-sauti visivyo vya kimsingi kutoka katika lugha changizi.

Hali kadhalika, Smith (2006) anadokeza kuwa uchopekaji aghalabu hutumiwa kurekebisha silabi zenye miundo isiyopendelewa. Fauka ya hayo, mkabala huu wa Mlingano Chanzi hutambua kanuni zifuatazo za uaminifu: $MAX - SB$ ambayo huelekeza kuwa vipande-sauti vyote katika neno-changizi sharti vijitokeze katika neno lililotoholewa. $DEP - SB$ inasema kuwa vipande sauti vyote katika maneno yaliyotoholewa kwenda katika lugha pokezi, sharti viwe katika lugha changizi. Kwa mfano; maneno kama “data, albino, protozoa, malaria na fistula”, maneno haya yameweza kutoholewa katika lugha ya Kiswahili kutokana na nadharia ya Mlingano Chanzi ambayo hutambua kanuni za uaminifu wa $Max-SB$, ambayo huonesha vipande sauti vyote vimeweza kujitokeza kutoka katika lugha ya Kiingereza ambayo ndiyo lugha changizi kwenda katika lugha ya Kiswahili ambayo ndiyo lugha ya pokezi. Hivyo basi katika utafiti huu mchakato wa utohozi huongozwa na mikakati mbalimbali ya kifonolojia na kimofolojia, kuna mfanano mkubwa kati ya lugha-

pokezi ambayo ni Kiswahili na lugha-changizi ambayo ni Kiingereza. Hali hii inaelezeka kwenye mtazamo wa mlingano-chanzi kupitia kanuni yake ya uaminifu. Mbinu za kiutohozi zilizobainishwa ni: udondoshaji wa irabu katikati ya neno, uchopekaji wa irabu mwishoni mwa neno, mbinu ya utohoaji wa moja kwa moja bila mabadiiko, mbinu ya utohoaji wa moja kwa moja na mabadiliko ya matamshi, uingizaji wa irabu katikati ya neno, na udondoshaji wa konsonati katika konsonanti kikundi.

Baada ya kupitia maandiko hayo, mtafiti ameamua kutumia nadharia ya Mkabala wa Mlingano Chanzi ulioasisiwa na Smith (2006). Mtafiti ameamua kutumia nadharia hii kwani ni nadharia ambayo inatoa dira au inaruhusu mikakati mbalimbali ya kiutohozi wa mkopaji wa maneno pamoja na fasiri za kifonolojia. Hali kadhalika, mkabala huu unasisitiza kanuni ya uaminifu baina ya umbo-fikirika la lugha changizi na umbo-tamkwa katika lugha pokezi. Kwa hivyo, kuna ulinganifu kati ya umbo-fikirika la lugha changizi na umbo la neno lililotoholewa.

Hata hivyo, mkabalawa Mlingano Chanzi bado unaruhusu mikakati ya urekebishaji wa maneno yaliyotoholewa, kwenye harakati za utohozi. Kwa mfano, maneno ya lugha changizi (Kiingereza) “Conductor, Office na Officer” kwenye lugha pokezi (Kiswahili) linakuwa “Kondakta, Ofisi, na afisa”, hapa tumeona namna ambavyo maneno yaliyotoholewa kutoka katika lugha ya Kiingereza kwenda katika lugha ya Kiswahili jinsi yalivyorekebishwa ili yaweze kuendana na kanuni za lugha ya Kiswahili.

Vile vile nadharia hii ya Mlingano chanzi imeonesha athari za utohoaji wa maneno ya Kiingereza katika lugha ya Kiswahili kwa kuonesha namna ambavyo kuna

maneno ambayo yana mfuatano wa konsonanti unaokubalika katika lugha ya Kiswahili, miongoni mwa maneno hayo ni kama vile; “benki, zinki, spingi, brashi na sketi, haya ni maneno ya Kiingereza ambayo yamechukua konsonanti ambatano kama zilivyo na kuzitumia katika lugha ya Kiswahili kwa kuziwekea irabu ambazo zinazoeendana na kanuni za utamkaji wa lugha husika ambayo ni Kiswahili, ambapo kwa mujibu wa nadharia ya Mlingano chanzi inaruhusu mchakato huo wa urekebishwaji wa maneno kutoka lugha changizi kwenda lugha pokezi.

Kwa ujumla katika utafiti huu nadharia ya Mlingano chanzi imetumika katika kubainisha mbinu za utohozi wa maneno ya Kiingereza katika Kiswahili pamoja na kuonesha athari za utohoaji wa maneno ya Kiingereza katika lugha ya Kiswahili.

2.6 Hitimisho

Katika sura hii, mtafiti amezungumzia mapitio mbalimbali yanayohusu utohoaji wa maneno kutoka lugha moja kwenda katika lugha nyengine (lugha changizi kwenda katika lugha pokezi).

Pia mtafiti ameonesha pengo la utafiti ambalo ni changamoto za utohoaji wa maneno ya Kiingereza kwenda katika lugha ya Kiswahili, ambapo kazi mbalimbali tangulizi hazikuonesha changamoto hizo za utohoaji.

Na mwisho kabissa mtafiti ameonesha nadharia ya Mlingano chanzi namna ambavyo imeweza kutumika kama dira katika kuonesha mchakato mzima wa utohoaji wa lugha moja kwenda katika lugha nyengine, na katika utafiti huu tumeweza kuona mbinu mbalimbali za utohoaji wa maneno ya Kiingereza kwenda katika lugha ya Kiswahili.

SURA YA TATU

MBINU ZA UTAFITI

3.1 Utangulizi

Katika Sura hii mtafiti ameeleza aina ya utafiti, eneo la utafiti, sampuli na usampulishaji wa utafiti pamoja na mbinu za kukusanyia data. Aidha katika sehemu hii mtafiti ameelezea mbinu zilizotumika kuchanganua data, namna ya udhibiti wa data na jinsi ulivyofanyika nahitimisho.

3.2 Eneo la Utafiti

Utafiti huu ulifanyikia katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, katika Taasisi ya Taaluma za Kiswahili (TATAKI). TATAKI ni miongoni mwa taasisi kongwe za lugha nchini Tanzania ambayo madhumuni yake ni kusimamia usanifishaji na maendeleo ya lugha ya Kiswahili nchini Tanzania. Chimbuko la TATAKI ni Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI). Mwaka 2009, TUKI iliungana na iliyokuwa Idara ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na kuunda Taasisi kubwa zaidi inayoitwa Taasisi ya Taaluma za Kiswahili – (TATAKI). Pia eneo lingine ambalo utafiti huu ulifanyika ni Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA), ambapo Baraza hili liliundwa na serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa lengo la kufuatilia na kusaidia ukuzaji wa Kiswahili ndani na nje ya nchi. Sababu ya mtafiti kuchagua maeneo hayo ni kutokana na vyombo hivyo kushughulikia maendeleo ya Kiswahili hapa nchini. Hivyo, mtafiti anaamini wataalamu katika taasisi hizi wana taarifa za kutosha na sahihi kuhusu mada ya utafiti huu.

3.3 Usampulishaji

Usampulishaji ni utaratibu wa kuchagua idadi ndogo ya wahusika kutoka katika kundi kubwa la watu ili watumike katika kuwafanyia utafiti badala ya kundi kubwa.

Katika utafiti huu, mtafiti alitumia mbinu kuu mbili za usampulishaji ambazo ni usampulishaji nasibu na usampulishaji usio nasibu.

3.3.1 Usampulishaji Nasibu

Kombo na Tromp (2006) wanasema, usampulishaji nasibu ni mchakato wa kuteua sampuli, ambapo kila sampuli katika idadi ya watafitiwa huwa na nafasi sawa ya kuchaguliwa. Usampulishaji nasibu ulitumiwa na mtafiti kwani aina hii ya usampulishaji ni mzuri katika kuondoa upendeleo wa uteuzi wa sampuli ya watafitiwa. Mtafiti alitumia mbinu hii kuwapata wafanyakazi wa taasisi zilizopendekezwa za BAKITA na TATAKI ambazo zilihusika katika utafiti huu, hivyo basi, usampulishaji nasibu ulikusudiwa na mtafiti kwa kwenda eneo husika na kuwakusudia wafanyakazi wa taasisi wa baraza la Kiswahili la Taifa na taasisi ya taaluma ya Kiswahili.

Kothari (2004) anasema, usampulishaji nasibu unampa nafasi kila mtu katika walengwa kuwa na fursa sawa ya kuteuliwa kuwa sampuli ya utafiti. Katika ukusanyaji data, mtafiti alitumia mbinu hii katika kuchagua watafitiwa husika kwani kila mtu atakuwa na fursa sawa ya kujieleza kama mwingine.

3.3.2 Usampulishaji Usio Nasibu

Mbinu ya pili ya usampulishaji iliyotumika ni usampulishaji usio nasibu. Mtafiti alitumia mbinu ya uteuzi usio nasibu ili kuwapata watafitiwa watakapo watakapo toa taarifa kwa mtafiti. Baada ya mtafiti kutumia usampulishaji nasibu kwa kuwakusudia waatafitiwa hao husika (BAKITA na TATAKI), alitumia mbinu hii kwa sababu watafitiwa walikua ni wachache, hivyo hakukua na haja ya kufanya uteuzi wa kundi maalum, na badala yake muhusika yeyote yule kutoka BAKITA

na TATAKI aliweza kufikiwa na mtafiti na kuweza kukusanya data zake kwa njia ya dodoso na hojaji, ambapo mtafiti aliweza kufanikisha utafiti wake kwa kupata ushirikiano kutoka kwao watafitiwa.

3.4 Sampuli

Babbie (2005) anaeleza kuwa, sampuli ni kundi dogo la watafitiwa linalochaguliwa katika kundi kubwa, ambalo ndilo hutoa data za kuwakilisha kundi zima. Kothari (2004) anafafanua sampuli ni kundi dogo la watafitiwa lililochaguliwa kuwakilisha sifa na tabia za kundi zima ambalo humsaidia mtafiti kupata taarifa kutoka sampuli hiyo ili kutoa majumuisho ya utafiti wake. Watafitiwa ni dhana inayotumiwa katika taaluma ya utafiti kurejelea watu au vitu vinavyoteuliwa na kuchaguliwa na mtafiti kwa ajili ya kufanyia utafiti wake, kwa kuzingatia malengo ya utafiti anaokusudia kufanya. Mchakato wa kuteuwa sampuli kutoka katika kundi lengwa inajulikana kama mbinu ya uteuzi wa sampuli. Kwa hivyo mtafiti amefanya uteuzi wa sampuli au usampulishaji kwa kuteua sampuli au kundi dogo la wawakilishi lililotumika katika utafiti ihuu.

Mtafiti aliwateua watafitiwa kwa kuzingatia uwezo wa taaluma zao za watafitiwa katika kutoa data zitakazohitajika kwa mujibu wa mada husika. Kwa ujumla, watafitiwa wote walikuwa arobaini na tano tu (45), kutokana na ikama (idadi) ya wafanyakazi waliopo BAKITA, na TATAKI, ambapo iadadi hiyo haikuwezi kuathiri upatikanaji wa data na uchanganuzi wa data kama Jedwali namba 3.1 linavyoonesha

Jedwali 3.1: Sampuli Iliyokusudiwa

Jinsia	Idadi	Asilimia
BAKITA	20	44.4
TATAKI	25	55.6
Jumla	45	100

Chanzo: Mtafiti (2019)

3.5 Mchanganuo wa Wahojiwa

Watafitiwa waliohusika katika utafiti huu walitoka katika taasisi za BAKITA, na TATAKI ambao wote walipatikana jijini Dar es Salaam. Katika utafiti huu, mtafiti alilenga kuwafikia watu 45 lakini baada ya kwenda katika eneo la utafiti, watafitiwa waliohusika walikuwa 43 ambao ni sawa na asilimia 95.5% ya watafitiwa wote waliokusudiwa. Watafitiwa 2 hawakuweza kushiriki katika utafiti huu kutokana na sababu zilizo kuwa nje ya uwezo wao, lakini kwa namna moja ama nyingine kupungua kwa idadi hiyo ya watafitiwa, ambayo ni sawa na asilimia 4.5% hakukuathiri upatikanaji na uchambuzi wa data.

3.6 Mbinu za Kukusanyia Data

Utafiti huu ulitumia mbinu mbili za kukusanyia data ambazo ni mahojiano na hojaji/dodoso.

3.6.1 Mbinu ya Mahojiano

Kombo na Tromp (2006) wanasema mahojiano ni majibizano ya ana kwa ana kati ya watu wawili au zaidi kwa lengo la kukusanya taarifa au maoni kuhusu suala fulani la kiutafiti lililoainishwa. Kwa mujibu wa Kothari (2009), mahojiano ya ana kwa ana ni

mbinu ambayo mtafiti huwauliza watafitiwa maswali na wakati mwingine watafitiwa nao huuliza maswali na mtafiti kutoa ufafanuzi. Mbinu hii ilitumika kukusanyia data kutoka kwenye eneo la utafiti, ambapo mtafiti alikutana na wataalamu wa lugha ya Kiswahili kutoka katika taasisi ya BAKITA na TATAKI, wataalamu hao walihojiwa na mtafiti na kutoa ushirikiano katika kuifanikisha kazi hii ya utafiti. Kwa kutumia mbinu ya mahojiano mtafiti alipata taarifa nyingi alizozihitaji kwa urahisi zaidi. Hili limewezekana kwani mbinu ya mahojiano ni nyepesi kupokea mabadiliko ya papo kwa papo bila kuathiri lengo la utafiti.

3.6.2 Mbinu ya Dodoso

Kothari (2004) anasema hojaji ni mbinu ya kukusanyia data ambayo mtafiti huandika maswali na baadaye huwapa watoa taarifa ili wayajibu na kumrudishia mtafiti. Williman (2011) anaeleza kuwa kuna maswali ya hojaji ya aina mbili. Aina ya kwanza ni maswali funge ambayo hutoa fursa kwa watafitiwa wa kuchagua jawabu. Aina hii ni rahisi kujibu na kuchanganua. Pia, inasaidia kupata majibu mahususi na huepusha upendeleo. Aina ya pili ya maswali ya hojaji ni maswali yasiyofunge, ambayo hutoa fursa au uhuru kwa watafitiwa kueleza kwa kina kile wanachokijua. Aidha, husaidia kupata taarifa nyingi zaidi kwani mtafitiwa hupewa nafasi ambapo huwa peke yake wakati anajibu maswali. Katika utafiti huu, mtafiti alitumia aina zote mbili za maswali, yaani maswali funge na maswali yasiyofunge. Mtafiti alichanganya aina zote za maswali kwa lengo la kuepuka mapungufu yanayoweza kutokea katika mbinu hizi mbili, ikizingatia kuwa kila moja ina mapungufu na ubora wake. Mtafiti alitoa maelekezo ya namna ya kujibu madodoso ili kuondoa wasiwasi kwa watafitiwa.

Mtafiti aligawa hojaji kwa watafitiwa ambao ni wafanyakazi wa taasisi za BAKITA na TATAKI ili wazijaze kwa muda uliopendekezwa. Wakati wahojiwa wakijibu maswali, mtafiti alikuwepo eneo la tukio ili kutoa msaada na ufafanuzi endapo utahitajika, lakini pia alikuwepo kuhakikisha kuwa maswali yote ya dodoso yanajibiwa. Mbinu ya hojaji ilichaguliwa kwa sababu inafaa sana katika kukusanya data katika kundi kubwa la watu na kwa muda mfupi sana hasa hojaji za papo kwa papo. Aidha, ni njia rahisi na ya haraka katika kukusanya na kuchanganua data.

3.7 Mbinu za Kuchanganua Data

Katika utafiti huu data zilichanganuliwa kwa kutumia aina mbili za mikabala. Mikabala hiyo ni mkabala wa kiidadi na mkabala usio wa kiidadi. Williman (1999) anasema kuwa mkabala wa kiidadi ni mbinu ya kuchanganua data ambayo mtafiti hutumia namba kurekodi taarifa na kuchanganuliwa kwa kutumia mbinu za kitakwimu. Kwa kawaida mtafiti hutumia achano sanifu ili kuchanganua data. Enon (1998) anasema kuwa, mkabala usio wa kiidadi ni mbinu mojawapo ya kuchanganua data ambayo mtafiti hueleza na kufafanua data zake kwa kutumia maelezo aliyoyapata kutoka kwenye eneo la utafiti. Aidha, Kress (2008) anafafanua mkabala huu kuwa, unaelezea vipi na kwa nini matukio yametokea. Katika utafiti huu, mtafiti alitumia mikabala yote miwili, yaani mkabala wa kiidadi na usio wa kiidadi.

Data za utafiti zilizokusanywa kwa njia ya mahojiano, na hojaji zilichanganuliwa kwa kutumia njia za kimaielezo na kiidadi. Njia ya kimaielezo ilitumika kuelezea changamoto za utohoaji wa maneno ya Kiingereza na kuyaingiza kwenye lugha ya Kiswahili. Matokeo yaliyopatikana yaliwasilishwa katika muundo wa majedwali. Lakini pia njia ya kitakwimu ilitumika katika lengo la pili linaloonesha athari za

utohoaji wa maneno ya Kingereza katika lugha ya Kiswahili, pamoja na lengo la tatu linaloonesha changamoto za utohoaji wa maneno ya Kingereza katika lugha ya Kiswahili ambapo njia hiyo ilioonesha namna takwimu za wataftiwa zilivyoweza kuchangia upatikanaji wa data.

Uwasilishaji na uchambuzi wa data ulifanyika kwa kuzingatia malengo mahususi ya utafiti wa mada hii na maswali yanayoambatana na malengo hayo. Aidha, baada ya kuzikusanya na kuzipanga data zilizopatikana kutoka kwenye majedwali ziliingia katika hatua ya uchambuzi ili kumsaidia mtafiti kuweza kuona ukweli unaotawala katika data hizo ambazo nazo hatimaye kupata msimamo sahihi kuhusu mada ya utafiti huu. Kwa mantiki hiyo, mbinu zifuatazo zilitumika; kwanza, kuunda majedwali yaliyomwezesha mtafiti kupata takwimu zilizopelekea kufikia malengo mahususi ya utafiti huu. Pili, data zilizowasilishwa kwanjia ya maelezo, zililitolewa kwa kifupi huku zikiandamanishwa na majedwali yenye takwimu hasa asilimia ili kuwasilisha data ya kutegemewa. Majedwali yalikuwa muhimu katika kuwasilisha matokeo ya data za makundi mbalimbali kama wafanyakazi na viongozi wataasisi.

3.8 Udhhabiti wa Data

Katika hatua hii mtafiti aliangalia vipengele vikuu viwili ambavyo nimbinu za kukusanyia data na kuaminika kwa data. Kothari (2004) anafafanua kwamba udhhabiti ni kiwango ambacho mbinu za utafiti zinapima kile kilichotakiwa kupimwa na mbinu hiyo. Sigh (2007) aliongeza kuwa zana au mbinu zote zilizotayarishwa kwa ajili ya kufanyia utafiti lazima zipimwe ili kuona kama zinafaa katika mazingira halisi yaliyokusudiwa. Katika utafiti huu mtafiti alilazimika kutumia hojaji na dodoso kwa kuwapatia wana idara zote mbili wa TATAKI katika chuo kikuu cha Dar Es Salaam

na BAKITA. Lengo la kuzipima hojaji na dodoso ilikuwa ni kujua iwapo maswali yanaeleweka kwa watafitiwa. Pia kujua iwapo mtafiti atapata taarifa anazozihitaji kulingana na utafiti wake. Baada ya kutumia hojaji na dodoso , mtafiti alibaini baadhi ya maneno ya kurekebisha na aliyarekebisha kwa kuondoa ugumu au kutoeleweka kwa swali husika. Hii ilimsaidia mtafiti kuwa na maswali yanayopimika, hivyo basi udhibiti wa data katika utafiti huu ulibainika pale ambapo mtafiti aliuliza maswali yanaoendana na malengo matatu ya utafiti huu ambayo ni; kubainisha changamoto za utohoaji wa maneno ya Kiingereza kwenda katika luha ya Kiswahili, kubainisha athari za utohoaji wa maneno ya Kiingereza katika lugha ya Kiswahili na Kufafanua changamoto za utohoaji wa maneno ya Kiingereza katika lugha Kiswahili. mtafiti uli

3.8.1 Kuaminika kwa Data

Best na Khan (2006) wanasema kuwa, kuaminika kwa data za utafiti kunatokana na uwezo wa mbinu za utafiti kuzalisha matokeo yale yale pale utafiti unaporudiwa kwa kutumia mbinu hizo. Kuaminika hujitokeza pale ambapo kuna uhusiano katika taarifa zilizotolewa na watu walewale wa muda tofauti (Furlong na Lovelace 2000). Katika utafiti huu kuaminika kwa data kulihakikiwa kwa kutumia mbinu za ukusanyaji wa data zilizoainishwa katika sehemu ya njia za ukusanyaji wa data hapo awali.

3.9 Hitimisho

Katika sura hii imebainisha kuwa utafiti huu ulifanyika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kitengo cha TATAKI na Baraza la Kiswahili la Taifa. Data za utafiti huu zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya mahojiano na mbinu ya hojaji /dodoso na

zilichanganuliwa kwa kutumia mikabala yote miwili, yaani mkabala wa kiidadi na usio wa kiidadi.

SURA YA NNE

UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA

4.1 Utangulizi

Sura hii inahusu uwasilishaji na uchambuzi wa data za utafiti. Uchambuzi wa data umefanywa kwa kuzingatia malengo mahsusi ya utafiti ambayo ni kubainisha mbinu za utohoaji wa maneno ya Kiingereza katika lugha ya Kiswahili, kuelezea athari za utohoaji wa maneno ya Kiingereza katika lugha ya Kiswahili, pamoja na kufafanua changamoto za utohoaji wa misamiati ya kiingereza katika lugha ya Kiswahili. Aidha, data zimechambuliwa kwa kuzingatia nadharia Mlingano Chanzi.

4.2 Mbinu za Utohoaji wa Maneno ya Kiingereza katika Lugha ya Kiswahili

Lengo la kwanza la utafiti huu ilikuwa ni kubainisha mbinu mbalimbali za utohoaji wa maneno ya lugha ya Kiingereza katika lugha ya Kiswahili. Katika ukusanyaji wa data mtafiti alitumia mbinu ya dodoso ambayo ilimwezesha kupata majibu ya swali la kwanza la utafiti huu ambalo lilihitaji kubaini mbinu za utohoaji wa maneno ya lugha ya Kiingereza kwenda lugha ya Kiswahili. Data zinaonesha kuwa kuna mbinu mbalimbali za utohoaji ambazo hutumika katika utohoaji wa maneno ya Kiingereza katika lugha ya Kiswahili kama zifuatazo:

4.2.1 Utohoaji wa Moja kwa Moja na Mabadiliko ya Matamshi

Miongoni mwa mbinu zinazotumika ni utohoaji wa moja kwa moja na mabadiliko ya matamshi unaofanyika katika utohoaji wa maneno kutoka katika lugha ya Kiingereza kwenda katika lugha ya Kiswahili. Data zinaonesha kuwa utohoaji wa aina hii unaweza kufanyika kwa kulichukua neno la lugha ya Kiingereza na kulifanyia mabadiliko katika matamshi ili yalingane na maneno ya lugha ya

Kiswahili. Mbinu hii ya utohoaji wa maneno kutoka katika lugha nyingine inaungwa mkono na Karekezi (2007:4) anayesema kuwa utohoaji ni kuchukua neno la kigeni na kulirekebisha ili lifanane kwa umbo, sauti na tabia ya lugha inayotohoa. Kwa mfano, neno la Kiingereza “budget” linatamkwa /bʌdʒit/, lakini lilipo toholewa kwenye lugha ya Kiswahili neno hilo linaandikwa “bajeti” na linatamkwa /baʒeti/ Mifano mingine ni kama inavyoonekana katika Jedwali 4.1.

Jedwali 4.1: Uthoaji wa Moja kwa Moja na Mabadiliko ya Matamshi

Kiingereza		Kiswahili	
Neno	Matamshi	Neno	Matamshi
Nut	/nʌt/	Nati	/na:ti/
Tropic	/ˈtrɒpɪk/	Tropiki	/trɒpiki/
Scale	/skeɪl/	Skeli	/ˈske:li/
Battery	/ˈbætri/	Betri	/ˈbe:tri/
Volcano	/vɒlˈkeɪn/	Volkano	/vɒlikano/
Budget	/bʌdʒɪt/	Bajeti	/baʒeti/
Switch	/swɪtʃ/	Swichi	/swi:tʃi/
Programme	/prəʊgræm/	Program	/prɔˈgra:mu/
Fuse	/fju:z/	Fyuzi	/ˈfju:zi/
Campaign	/kæmˈpeɪn/	Kampeni	/kampeni/
Management	/ˈmænɪdʒmənt/	Menejimenti	/menejment/
Case	/keɪs/	Kesi	/kɛsi/
Judge	/dʒʌdʒ/	Jaji	/ˈʒa:ʒi/
Gas	/gæs/	Gesi	/gesi/

Kiingereza		Kiswahili	
Neno	Matamshi	Neno	Matamshi
Register	/redʒɪstə/	Rejesta	/rɛʒɛstə/
Fen	/fæn/	Feni	/fɛni/
Cake	/keɪk/	Keki	/ˈkɛ:ki/
Carbon	/ˈkɑ:bən/	Kaboni	/ˈkɑbɔni/
Hydrogen	/ˈhaɪdrədʒən/	Haidrojeni	/hajɪdrɔˈʒɛni/
Naitrogen	/ˈnaɪtrədʒən/	Naitrojeni	/nɪtrɔˈʒɛni/
Silicon	/ˈsɪlɪkəʊn/	Silikoni	/ˈsɪlɪkɔni/
Adapter	/əˈdæptər/	Adapta	/ɑ:dapta/
Picture	/ˈpɪktʃər/	Picha	/ˈpɪtʃɑ/
Lorry	/lɔri/	Lori	/ˈlɔ:ri/
Driver	/draɪvər/	Dereva	/dɛˈrevɑ/
Helicopter	/ˈhelɪkɒptər/	Helikopta	/helɪkɒptɑ/
Police	/pəˈli:s/	Polisi	/pɔˈlisi/
Conductor	/kənˈdʌktər/	Condakta	/kɔˈndakta/
Shilling	/ˈʃɪlɪŋ/	Shilingi	/ʃɪˈlɪŋgi/
Billion	/ˈbɪljən/	Million	/bɪliˈjɔni/
Week	/wi:k/	Wiki	/w:ki/
Report	/rɪˈpɔ:t/	Ripoti	/rɪpɔ:ti/
Ward	/wɔ:d/	Wodi	/ˈwɔdi/
Doller	/ˈdɒləɹ/	Dola	/ˈdɔ:la/
Office	/ɔfis/	Ofisi	/ɔˈfisi/

Chanzo: Mtafiti (2019)

Hivyo basi kutokana na Jedwali 4.1 data za utafiti zinaonesha kuwa mbinu hii hutumika kwa kufanya marekebisho kutoka katika muundo wa lugha ya Kiingereza. Kinachofanyika katika mbinu hii ni kuandika sauti za neno la Kiingereza kwa kutumia konsonanti za lugha ya Kiswahili. Kwa hiyo maneno yote hutamkwa kwa sauti inayofanana kulingana na lafudhi ya lugha husika, lakini utofauti utajitokeza jinsi neno linavyoandikwa, msingi wa kufanya hivyo wa kuchukua sauti ya maneno ya lugha changizi na kuyaandika katika kughu pokezi ni kuyafanya maneno hayo yaendane na kanuni za lugha husika ambayo ni Kiswahili.

Data za utafiti (Rejea 4.1) linaendana pia na matakwa ya Nadhari ya Mlingano Chanzi ambayo inaruhusu mikakati ya urekebishaji wa maneno ya utohozi kama inavyoonekana kwenye jedwali 4.1.

4.2.2 Utohoaji wa Moja kwa Moja Bila Mabadiliko

Data za utafiti zinaonesha kuwa katika mbinu hii ya utohoaji neno huchukuliwa jinsi lilivyo kimuundo na kimaana kutoka katika lugha changizi. Watafitiwa 20 kati ya 23 ambayo ni sawa na 87% ya watafitiwa wote waliohusika kutoka TATAKI walisema kuwa, kwa kawaida maneno yanayofanyiwa utohoaji wa moja kwa moja bila mabadiliko ni sharti yaweze kushabihiana na mwenendo wa maumbo ya maneno ya lugha ya Kiswahili (lugha pokezi). Hii ina maana kwamba maneno yaliyotoholewa kwa mbinu hii, inakuwa nyepesi zaidi ukilinganisha na maneno yanayoingia yakiwa na umbo tofauti na lugha ya Kiswahili. Jedwali namba 4.2 linaonesha maneno yaliyotoholewa kwa mbinu ya moja kwa moja bila mabadiliko.

Jedwali 4.2 Utohoajiwa Moja kwa Moja bila Mabadiliko

Neno la Kiingereza	Matamshi ya Kiingereza	Neno la Kiswahili	Matamshi ya Kiswahili
Fistula	/`fɪstjʊlə/	Fistula	/fɪstjula/
Malaria	/mə`leəriə/	Malaria	/malarija/
Albino	/`ælbɪ:nʊə/	Albino	/albino/
Data	/`deɪtə/	Data	/`da:ta/
Protozoa	/prəʊtə`zəʊə/	Protozoa	/protozə/
Drama	/`dra:mə/	Drama	/drama/

Chanzo: Mtafiti (2019)

Kwa mujibu wa Nadharia ya Mlinganyo Chanzi, mahusiano ya lugha changizi na lugha pokezi yanatokea kwa kulingana baina ya umbo tamkwa (la lugha pokezi) na umbo-fikirika (unaotokana na lugha changizi). Hivyo basi, kwa kutumia nadharia hii inasisitiza kwamba vipengele vyote vya umbo la lugha changizi sharti vijitokeze katika umbo la lugha pokezi, ndiyo maana kwa kupitia mifano iliyopo katika Jedwali 4.2 linaonesha namna ambavyo lugha pokezi ilivyoweza kutohoa maneno kutoka katika lugha ya Kiingereza bila mabadiliko katika maumbo yake, lakini utofauti hujitokeza katika matamshi ya lugha ya Kiingereza na lugha ya Kiswahili.

Data za utafiti (Rejea 4.2) linaendana pia na matakwa ya Nadhari ya Mlingano Chanzi inasisitiza kwamba vipengele vyote vya umbo la lugha changizi (Kiingereza) sharti vijitokeze katika umbo la lugha pokezi (Kiswahili). Kwa mfano, msamiati wa lugha changizi (Kiingereza) “Albino, Data, na Drama” kwenye lugha pokezi (Kiswahili) linakuwa “Albino, Data, na Drama”.

4.2.3 Udondoshwaji wa Irabu Katikati ya neno

Data za utafiti zinaonesha kuwa udondoshwaji wa irabu ni miongoni mwa mbinu ambayo hutumiwa katika utohoaji wa maneno ya Kiingereza. Katika mbinu hii utohoaji hufanyika kwa kudondosha baadhi ya irabu katikati mwa neno. Kwa kutetea hoja hii, watafitiwa 21 kati ya 23 kutoka TATAKI ambao ni sawa na 91% walisema kuwa mbinu ya udondoshaji wa irabu inaweza kutokea katikati mwa neno ili kuweza kukidhi mahitaji ya lugha pokezi, Katika mbinu hii ya utohoaji, mahusiano ya lugha changizi na lugha pokezi yanabainika kwa kulingana baina ya umbo- tamkwa (la lugha pokezi) na umbo-fikirika (unaotokana na lugha changizi). Kwa hiyo, vipengele vyote vya umbo la lugha changizi sharti vijitokeze katika umbo la lugha pokezi. Kwa mfano, neno “Chief” linakuwa “Chifu”, neno “boat” linakuwa “boti”. Hata hivyo, Nadharia ya Mlingano Chanzi bado inaruhusu mikakati ya urekebishaji wa maneno yaliotoholewa kwenye harakati za utohozi ili kukidhi mahitaji ya lugha husika kwa kufuata taratibu na kanuni za lugha hiyo.

Nadharia hii inaonesha kuwa umbo fikirika la lugha changizi, hujengeka kutokana na ujuzi wa tahajia wa lugha hiyo, uelewa wa sarufi ya lugha changizi, pamoja na fikra alizonazo mkopaji kuhusu lugha changizi. Umbo hili fikirika si lazima lifanane na umbo la neno linalotokana na lugha changizi, kwa mfano “speaker” na kuwa “spika”, team linakua “timu”, “Anaemia” na kuwa “anemia”. Mifano hii imeweza kutuonesha mabadiliko ya umbo fikirika (pokezi) jinsi lilivyoweza kudondosha irabu “ea” na kuchepeka irabu “i” ,na kudondosha irabu “a” katika mfano wa “Anaemia” kutoka katika lugha ya Kiingereza. Msingi wa kufanya hivyo ni kukidhi kanuni za lugha pokezi. Lengo la kudondosha irabu katikati mwa neno ilikuwa ni kuondoa utaratibu

wa lugha ya Kiingereza katika utamkaji wake, na kuupeleka katika utaratibu wa lugha ya Kiswahili, tuangalie Jedwali 4.3.

Jedwali 4.3 Udondoshaji wa Irabu katikati ya neno

Neno la Kiingereza	Matamshi ya Kiingereza	Neno la Kiswahili	Matamshi ya kiswahili
Boat	/bəʊt/	Boti	/bɔti/
Chief	/tʃi:f/	Chifu	/tʃifu/
Team	/ti:m/	Timu	/timu/
Anaemia	/əˈni:miə/	Anemia	/anɛmija/
Speaker	/ˈspi:kə/	Spika	/spika/
Campaign	/kæmp`peɪn/	Kampeni	/kampeni/

Chanzo: Mtafiti (2019)

4.2.4 Uingizaji wa Irabu Mwishoni mwa Neno

Data kutoka katika eneo la utafiti zinaonesha kuwa, miongoni mwa mbinu ambazo hutumiwa na watohoaji wa maneno ya lugha ya Kiswahili kutoka kwenye maneno ya lugha ya Kiingereza ni uingizaji wa irabu mwishoni mwa neno, watafitiwa 19 kati ya 20 sawa na 95% kutoka BAKITA, wamesema uingizaji wa irabu kwenye neno la Kiswahili hufanyika kwa kuingiza irabu kutoka katika lugha changizi. Katika Jedwali namba 4.4 linaonesha mifano mbalimbali ya uingizaji wa irabu mwishoni mwa neno. Madhumuni ya kufanya hivyo ni kutaka kuwe na mfuatano wa konsonanti na irabu ili uweze kuendana na utaratibu wa lugha ya Kiswahili. Hivyo basi, data katika sehemu hii inatuonesha kuwa irabu inaongezeka mwishoni, kwa kutegemea neno la lugha husika linavyohitaji irabu ili likidhi mahitaji ya lugha ya Kiswahili.

Jedwali 4.4 Uingizaji wa Irabu Mwishoni mwa Neno

Neno la Kiingereza	Matamshi ya Kiingereza	Neno la Kiswahili	Matamshi ya Kiswahili
Pencil	/ˈpensl/	Penseli	/penseli/
Kilogram	/ˈklɒgræm/	Kilogramu	/kilogramu/
Jam	/dʒæm/	Jamu	/jamu/
Bom	/bɒm:/	Bomu	/bɒmu/
Pin	/pɪn/	Pini	/pini/
Card	/kɑːrd/	Kadi	/ˈkadi/
Shilling	/ˈʃɪlɪŋ/	Shilingi	/ʃɪˈlɪŋgi/
Billion	/ˈbɪljən/	Bilioni	biliˈjɔni/
Million	/ˈmɪljən/	Milioni	/miliˈjɔːni/
Professor	/prəˈfesər/	Profesa	/prɔˈfɛːsə/
Report	/rɪˈpɔːt/	Ripoti	/ripɔːti/
Doller	/ˈdɒlər/	Dola	/ˈdɔːlə/
Ward	/wɔːd/	Wodi	/ˈwɔdi/
Carbon	/ˈkɑːbən/	Kaboni	/ˈkɑbɔni/
Hydrogen	/ˈhaɪdrədʒən/	Haidrojeni	/hajidrɔˈjɛni/
Naitrogen	/ˈnaɪtrədʒən/	Naitrojeni	/nitɔˈjɛni/
Silcon	/ˈsɪlɪkəʊn/	Silikoni	/ˈsɪlɪkɔni/
Conductor	/kənˈdʌktər/	Condakta	/kɔˈndakta/

Chanzo: Mtafiti (2019)

Sambamba na hilo pia, uingizaji wa irabu mwishoni mwa neno/maneno yanayoishia na sauti /a,,i,o,u/. Utaratibu huo wa kuingiza irabu mwishoni mwa neno kwenye lugha ya Kiswahili, ni kukidhi haja ya lugha pokezi kwa maneno yanayotokana na

lugha ya Kiingereza. Hali kadhalika, Smith (2006) anadokeza kuwa uingizaji wa irabu aghalabu hutumiwa kurekebisha muundo kutoka katika lugha changizi na kuupeleka katika lugha pokezi. Nadharia ya Mlingano Chanzi hutambua kanuni zifuatazo za uaminifu: *MAX – SB* ambayo huelekeza kuwa vipande-sauti vyote katika neno- changizi sharti vijitokeze katika neno lililotoholewa, dai hili lina maana kuwa, vipande sauti vya lugha ya Kiingereza ambayo ndiyo inayotoholewa, sharti vipande sauti hivyo vijitokeze katika lugha ya Kiswahili.

Data za utafiti zinaonesha kuwa, irabu inayoongezwa mwishoni mwa neno hutegemea neno linavyotamkwa ili kuendana na utaratibu wa lugha ya Kiswahili wa kuandika maneno sawasawa na yanavyotamkwa. Dhana hii pia inaungwa mkono na nadharia ya Mlingano Chanzi ambayo imetumika katika utafiti.

4.2.5 Uingizaji wa Irabu Katikati ya Neno

Mtafiti ameweza kubaini baadhi ya maneno yanayotoholewa kwa kupitia mbinu ya uchopekaji wa irabu katikati mwa neno, mbinu hii imebainishwa na watafitiwa 18 kati ya 20 sawa na 90% kutoka katika eneo la utafiti BAKITA, ambapo data za utafiti zinaonesha namna irabu inavyochopekwa katikati mwa neno ambalo limetoholewa kutoka katika lugha ya Kiingereza. Jedwali namba 4.5 linaonesha namna ambavyo irabu zilivyochopokwa na kudondosha baadhi ya konsonanti na hata pia kuzibadili baadhi ya irabu kutoka katika maneno ya lugha changizi (Kiingereza). Kwa mujibu wa Nadharia ya Mlingano Chanzi inaruhusu mkakati wa urekebishaji wa maneno kuoka lugha changizi kwenda na kwenda katika lugha pokezi ambayo ni Kiswahili.

Jedwali 4.5: Uingizaji wa Irabu katikati ya neno

Neno la Kiingereza	Matamshi ya Kiingereza	Neno la Kiswahili	Matamshi ya Kiswahili
Passport	/pa:spɔ:t/	Pasipoti	/pasipɔti/
Film	/film/	Filamu	/filamu/

Chanzo: Mtafiti (2019)

4.2.6 Udondoshaji wa konsonanti katika Konsonanti kikundi

Data za utafiti zinaonesha kuwa utohoaji wa maneno ya Kiswahili kutoka katika maneno ya Kiingereza huweza kufanyika kwa kutumia mbinu ya udondoshaji wa konsonanti katika neno. Waafitiwa 19 kati ya 20, ambapo ni sawa na 95% kutoka BAKITA, data zinaonesha kuwa, mchakato wa udondoshaji wa konsonanti hufanyika pale ambapo mpangilio wa konsonanti hizo umekiuka taratibu ya lugha ya Kiswahili, kiasi cha kusababisha ugumu wa kuligawa neno hilo katika silabi zenye kutamkika kwa lugha Kiswahili. Mtafiti aliendelea kusema kuwa utohoaji wa udondoshaji wa konsonanti huweza kufanyika katikati na mwishoni mwa neno.

Lakini pia, mbinu ya udondoshaji hufanyika ili kuweka ulinganifu kati ya umbo-fikirika la lugha changizi na umbo la neno lililotoholewa. Nadharia hii ya Mlingano chanzi inaruhusu mikakati mbalimbali urekebishaji wa maneno yaliotoholewa, mfano neno “Passport” limetoholewa na kuwa “Pasipoti”, Organ limetoholewa na kuwa ogani, Lorry limetoholewa na kuwa lori”, hapa tumeona nmna ambavyo kuna mfuatano wa konsonanti zaidi ya mbili kutoka katika lugha ya Kiingereza na kudondosha miongoni mwa konsonanti hizo ili kukidhi mahitajio ya lugha inayotohoa. Hivyo badi nadharia hii inasisitiza kanuni ya uaminifu baina ya umbo-

fikirika la lugha changizi na umbo-tamkwa katika lugha pokezi. Kwa hivyo, kuna ulinganifu kati ya umbo-fikirika la lugha changizi na umbo la neno lililotoholewa. Jedwali namba 4.6 linaonesha maneno ambayo konsonanti kikundi zimedondoshwa.

Jedwali 4.6 Udondoshaji wa Konsonanti katika Konsonanti Kikundi

Neno la Kiingereza	Matamshi ya Kiingereza	Neno la Kiswahili	Matamshi ya kiswahili
Passport	/pa:spɔ:t/	Pasipoti	/pasipɔti/
Organ	/ˈɔ:gən/	Ogani	/ɔgani/
Rubber	/ˈrʌbə/	Raba	/raba/
Artery	/ˈa:təri/	Ateri	/ateri/
Officer	/ɔfisə/	Afisa	/afisa/
Lorry	/lɔri/	Lori	/ˈlɔ::ri/
Office	/ɔfis/	Ofisi	/ɔ'fisi/
Shilling	/ˈʃɪlɪŋ/	Shilingi	/ʃɪ'lingi/
Billion	/ˈbɪljən/	Bilioni	bili'jɔni/
Million	/ˈmɪljən/	Milioni	/mili'jɔ::ni/
Professor	/prə'fesər/	Profesa	/prɔ'fɛ:sa/

Chanzo: Mtafiti (2019)

Matokeo haya yanajibu swali la kwanza la utafiti ambalo ni kubaini mbinu zinazotumika katika utohoaji wa maneno ya Kiingereza katika lugha ya Kiswahili, lakini pia wakati huohuo kukamilisha lengo la kwanza la utafiti huu. Kwa ujumla, data za utafiti zinaonesha kuwa mbinu za utohozi zinazotumika katika Kiswahili ni utohoaji wa moja kwa moja bila mabadiliko, utohoaji wa moja kwa moja na

mabadiliko ya matamshi, uongezaji wa irabu mwishoni, undondoshwaji wa irabu katikati ya neno, na udondoshaji wa konsonanti katika konsonanti kikundi.

4.3 Athari za Utohoaji wa Maneno ya Kiingereza katika Lugha ya Kiswahili

Lengo la pili la utafiti huu ni kueleza athari za utohoaji wa maneno ya Kiingereza katika lugha ya Kiswahili, ambapo lengo hili limetumia mbinu ya hojaji kuweza kukusanyia data, ambayo imeweza pia kujibu swali la athari zipi zinazoweza kujitokeza wakati wa utohoaji wa maneno ya Kiingereza katika lugha ya Kiswahili. Data za utafiti zinaonesha kuwa kuna athari mbalimbali ambazo zimeweza kujitokeza katika utohoaji wa maneno ya lugha ya Kiingereza kwenda katika lugha ya Kiswahili kama ifuatavyo:-

4.3.1 Ukuzaji wa Msamiati wa Lugha ya Kiswahili

Data kutoka eneo la utafiti zinaonesha kuwa, utohoaji kutoka lugha ya Kiingereza umesababisha msamiati wa Kiswahili kuongezeka kutokana na ukuaji wa sayansi na teknonojia, ambapo ukuaji huo husababisha ongezeko la msamiati wa Kiingereza katika lugha ya Kiswahili, ambapo pia hupelekea kuongezeka kwa watumiaji wa lugha hiyo, msamiati wa lugha ukikua na watumiaji huongezeka wa lugha hiyo, hivyo basi kwa kutumia mbinu mbalimbali za kutohoa maneno ya Kiingereza kwenda katika Lugha ya Kiswahili, kuna maneno mbalimbali ambayo yalitoholewa na yanatumika katika sekta mbalimbali kama ifuatavyo;

4.3.1.1 Upande wa Afya

Mtafitiwa mmoja kutoka TATAKI alieleza kuwa, kwa upande wa afya utohoaji wa lugha ya Kiingereza kwenda katika lugha ya Kiswahili umesababisha kuwepo kwa maneno mengi yanayotumika katika sekta ya afya. Mtaalamu huyo aliweza

kuyaaanisha maneno yaliyotoholewa kutoka sekta ya afya kama vile; malaria, fistula, albino, ogani, protozoa, amonia, ateri, nyurosis, bendeji, naitrojeni, kaboni, haidrojeni, na kansa, ni maneno ambayo yamepatikana kwa kutoholewa kutoka katika lugha ya Kiingereza na kutumika katika lugha ya Kiswahili kwa kutumia mbinu tajwa hapo za utohoaji wa maneno.

4.3.1.2 Upande wa Elimu

Data za utafiti zinaonesha kuwa, utohoaji wa maneno ya lugha ya Kiswahili kutoka katika lugha ya Kiingereza, umewezesha upatikanaji wa maneno ambayo hutumiwa katika sekta ya Kielimu. Hoja hii ilifanuliwa na watafitiwa 18 kati ya 20 ambao ni sawa na 90% ya watafitiwa wote kutoka TATAKI, wakionesha kuwa, yapo maneno mbalimbali kutoka katika nyanja ya kielimu kama vile saikolojia, zuolojia, Fomyula, namba, fizikia, biolojia, jiografia, teknolojia, sosholojia, na leksikografia ambayo ni maneno yaliyopatikana kwa utohoaji wa msamiati kutoka lugha ya Kiingereza kwenda katika lugha ya Kiswahili.

4.3.1.3 Upande wa Biashara

Mtaalamu kutoka BAKITA alipohojiwa kuhusu athari za utohoaji, alijibu kuwa kuna maneno mengi yaliyotoholewa kutoka katika lugha ya Kiingereza na kutumiwa katika lugha ya Kiswahili, ambayo yanatumika katika sekta ya biashara. Mtaalamu huyo ameonesha maneno ambayo hutumiwa katika sekta ya kibiashara ni kama vile benki, bajeti, akaunti, cheki na kilogramu. Hivyo basi, data za utafiti zinaonesha namna ambavyo lugha ilivyoweza kuiathiri lugha ya Kiswahili kwa kua na maneno mengi ya lugha ya Kiingereza, kwa kupitia mbinu mbalimbali za utohoaji, ambapo

lugha ikikua kimsamiati, husababisha kuwa na ongezeko la watumiaji wengi wa lugha hiyo katika sekta ya afya, kielimu na biashara.

4.3.2 Mfuatano wa Sauti Unaokubalika Katika Lugha ya Kiswahili.

Uchambuzi wa data unadhihirisha kuwa ipo mifuatano ya konsonanti katika lugha ya Kiingereza ambayo imeachwa iendeleo kutumika kwenye lugha ya Kiswahili. Data za utafiti zinaonesha kuwa mifuatano hiyo ni ile inayopatikana kwenye lugha ya Kiingereza na inayokubalika katika lugha ya Kiswahili na hatimaye kuacha athari katika matumizi ya lugha ya Kiswahili. Nadharia ya Mlingano chanzi (Smith 2006) inaeleza kuwa, mahusiano ya lugha changizi na lugha pokezi ambayo yanaonesha kuwa kuna kulingana baina ya lugha changizi na lugha pokezi. Kwa mantiki hii data za utafiti zimeonesha namna ambavyo lugha ya Kiswahili ilivyoweza kuathiriwa na lugha ya Kiingereza kwa kutumia mbinu mbalimbali za utohozi, tuangalie mifano ya maneno yaliyo katika Jedwali namba 4.7 yaliyopatikana kwenye eneo la utafiti;-

Jedwali 4.7: Mfuatano wa Sauti Unaokubalika Katika Lugha ya Kiswahili

Neno la Kiingereza	Matamshi ya Kiingereza	Neno la Kiswahili	Matamshi ya Kiswahili
Bank	/bæŋk/	Banki	/bɛŋki/
Zinc	/ziŋk/	Zinki	/zinki/
Bolt	/bɔlt/	Bolti	/bɔlti/
Spring	/sprɪŋ/	Springi	/springi/
Brush	/brʌʃ/	Brashi	/braʃ/
Skirt	/skɜ:rt/	Sketi	/sketi/

Chanzo: Mtafiti (2019)

4.4 Changamoto za Utohoaji wa Maneno ya Kiingereza katika lugha ya Kiswahili.

Lengo la tatu la utafiti huu lilikuwa kufafanua changamoto za utohoaji wa maneno kutoka katika lugha ya Kiingereza kwenda katika lugha ya Kiswahili, ampapo mbinu iliyotumika kukusanyia data ni mbinu ya dodoso, ambayo pia imeweza kujibu swali ambalo lilohitaji ufafanuzi wa changamoto zipi zinazoweza kujitokeza wakati wa utohoaji wa maneno ya Kiingereza katika lugha ya Kiswahili. Data za utafiti zinaonesha kuwa kuna changamoto mbalimbali ambazo zimejitokeza katika utohoaji wa maneno ya lugha ya Kiingereza kwenda katika lugha ya Kiswahili kama ifuatavyo;

4.4.1 Kudumaza Lugha

Watafitiwa 30 kati ya 43 ambao ni sawa na 70% ya watafitiwa wote waliohusika katika utafiti huu, walisema kuwa, kuna changamoto ambazo hutokea kwenye utohoaji wa maneno, kwa kupitia mbinu mbalimbali za utohoaji kama vile utohoaji wa moja kwa moja bila mabadiliko, kwa kupitia mbinu hii kwa namna moja ama nyengine hudumaza lugha inayotohoa. Data za utafiti zinaonesha kuwa katika mbinu hizo huifanya lugha ya Kiswahili kudumaa katika kupata maneno yake halisi. Kwa mfano maneno kama vile “Data, fistula, malaria, albino na protozoa”, ambayo yanatoka katika lugha ya Kiingereza, yanatokana katika mbinu ya utohoaji wa moja kwa moja bila ya mabadiliko, ambapo maneno tajwa hayo juu huandikwa kama yalivyo katika lugha ya Kiswahili, na mwishowe maneno hayo hayakuweza kupatiwa maneno yake halisi ya lugha ya Kiswahili, na badala yake yamechukuliwa kutoka katika lugha ya Kiingereza na kutumiwa kama yalivyo katika lugha ya

Kiswahili. Tofauti iliyopo hapo ni ya matamshi tu ya lugha ya Kiingereza na lugha ya Kiswahili. Kwa mantiki hii huidumaza lugha pokezi kwa kuwa hakuna mabadiliko katika muundo wake wa awali wa lugha changizi.

4.4.2 Ukiukwaji wa Kanuni ya Mkazo Katika Utamkwaji wa Maneno ya

Lugha ya Kiswahili.

Hoja hii iliungwa mkono na watafitiwa 39 kati ya 43 sawa na 91% ambapo data za utafiti zinaonesha kuwa kati ya changamoto za utohoaji zinazojitokeza ni pamoja na ubadilishaji wa maneno kwa kuweka mkazo usio wa kawaida katika lugha ya Kiswahili. Katika lugha ya Kiswahili mkazo hutokea katika silabi ya pili kutoka mwishoni mwa neno, tofauti na hali ilivyo katika lugha ya Kiingereza ambapo mkazo hujitokeza mwanzoni au katikati mwa neno. Katika utafiti huu, mtafiti ameweza kubaini kuwa si maneno yote yaliyotoholewa yameweza kufuata kanuni ya mkazo katika lugha ya Kiswahili. Maneno yaliyo na changamoto zaidi ni yale ambayo yaliyotoholewa kwa mbinu ya moja kwa moja na bila mabadiliko, hutumika kama yalivyo. Maneno hayo yaliyotoholewa kutoka katika lugha ya Kingereza na kutumika moja kwa moja katika lugha ya Kiswahili ni kama vile, (da'ta ,dra'ma ,proto'zoa, mala'ria na fis'tula), ambapo mkazo wake hujitokeza katika silabi ya pili kutoka mwisho wa neno, na pia kuna utofauti wa mkazo wa lugha ya Kingereza katika maneno hayo yanavyotamkwa kama vile, ('data) ('drama), (ma'laria), na (proto'zoa), hivyo tumeona utofauti wa mkazo namna unavyojitokeza katika lugha ya Kiingereza na lugha ya Kiswahili, ambapo kwa namna moja ama nyengine hudhihirisha changamoto ya uwekaji mkazo katika ya lugha hiyo pokezi, kwa kuwa kimuundo hakuna utofauti wowote uliojitokeza katika uwandishi wa maneno hayo.

Hata hivyo kimatamshi kuna utofauti kutokana na namna ya uwekaji mkazo ulio katika lugha ya Kingereza na lugha ya Kiswahili.

4.4.3 Changamoto ya Mfuatano wa Sauti Isiyo Katika Muundo wa Lugha ya Kiswahili

Akifafanua hoja hii mtaalamu mmoja kutoka TATAKI, alionesha kuwa, miongoni mwa changamoto za utohoaji wa maneno ya lugha ya Kiingereza katika lugha ya Kiswahili ni kuleta aina ngeni ya ruwaza katika lugha ya Kiswahili. Aliendelea kuonesha kuwa lugha ya Kiingereza ina changamoto za utohoaji wa maneno yake kwenda katika lugha ya Kiswahili, mifano kadhaa ambayo, mingi ilionesha herufi mbili zilizoambatana ambazo zenye mifuatano ya sauti ambayo haipo katika matumizi ya lugha ya Kiswahili. Mifuatano hiyo ya sauti ni kama vile , /ks/ kama ilivyo katika soksi /dk/ katika dikteta /kl/ katika klabu /br/ katika brashi, /kr/ katika elektroni, /nk/ na katika sinki/.

Kwa mujibu wa Smith,(2009) ambaye ni muasisi wa Nadharia ya Mlingano chanzi ulioongoza utafiti huu, yeye alisema kuwa inatakiwa kuwepo na mikakati mbalimbali ya kiutohozi, ambayo inatokana na uelewa wa mtohoaji. Pia anasisitiza kuwa kanuni ya uaminifu baina ya umbo-fikirika la lugha changizi na umbo-tamkwa katika lugha pokezi lazima izingatiwe. Kwa hivyo, kunatakiwa kuwepo na ulinganifu kati ya umbo- fikirika la lugha changizi, na umbo la neno lililotoholewa. Jedwali namba 4.8 linaonesha baadhi ya mifuatano ya herufi ambatano ambazo hazipo katika lugha ya Kiswahili, lakini zinatumiwa kwa baadhi ya maneno yaliyotoholewa kutoka katika lugha ya Kiingereza kwenda katika lugha ya Kiswahili.

**Jedwali 4.8: Changamoto ya Mfuatano wa Sauti isiyo Katika Muundo wa
Lugha ya Kiswahili**

Kiingereza	Herufi	Kiswahili
Socks	Ks	Soksi
Dictator	Dk	Dikteta
Club	Kl	Klabu
Brash	Br	Brashi
Electron	Ktr	Electroni
Sink	Nk	Sinki
Professor	Pr	Profesa
Nitrogen	Tr	Naitrojeni
Hydrogen	Dr	Haidrojeni

Chanzo Mtafit (2019)

Massamba (2004) anaeleza kwamba lugha ya Kiswahili ina mifuatano ya sauti zenye herufi ambatano, ambazo ni ch, dh, gh, , ng', ny, th, na sh. Hata hivyo, mtafitiwa mmoja kutoka BAKITA alisema kuwa, utohoaji huu hufanyika kwa lengo la kukidhi haja ya maneno mapya katika lugha ya Kiswahili, hivyo husababisha kuwepo kwa herufi ambatano mbalimbali ambazo hapo kabla hazikuwepo katika matumizi ya lugha ya Kiswahili. Hivyo kuwepo kwa mfuatano wa sauti isiyo katika lugha ya Kiswahili hupelekea kukiuka kanuni za lugha ya Kiswahili ambazo hazina mifuatano ya konsonanti iliyo ambatano katika lugha pokezi.

4.4.4 Kasumba ya Wazungumzaji wa Lugha ya Kiingereza

Changamoto nyingine inayoweza kutokea ni pale ambapo utohoaji wa lugha unapofanyika kwa wazungumzaji. Istilahi inaweza kutoholewa si kwa kuwa haipo katika lugha husika, bali kwa vile wenye istilahi inayotoholewa wanaonekana kuwa

na ustaarabu wa juu zaidi na kuonekana kuwa lugha yao ni bora zaidi. Kwa mfano matumizi ya maneno kama “feli” badala ya “shindwa”, “kona” badala ya “pembe”, “daktari” badala ya “mganga” Dai hili husababisha kasumba ya kuiona lugha changizi kuwa ni bora zaidi kuliko lugha pokezi.

4.4.5 Upungufu au Ufinyu wa Mbinu za Utohoaji

Data za utafiti zinaonesha kuwa kuna upungufu au ufinyu wa mbinu za utohoaji. Dai hili linathibitisha kuwa, kuna baadhi ya mbinu kama mbinu ya utohoaji wa moja kwa moja bila ya mabadiliko, ambayo haioneshi utafauti wa maneno yaliyotoholewa na badala yake mbinu hii imeweza kuhamisha maneno ya lugha ya changizi kwenda katika lugha ya Kiswahili kama yalivyo kimuundo, ambapo husababisha utohozi wake kutohoa miundo ya kifonolojia na kimofolojia ya lugha inayotohoa na hivyo kuonekana utohozi umefanyika bila ya kuwa na mabadiliko ya aina yoyote ile.

SURA YA TANO

MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.1 Utangulizi

Sura hii imejumuisha muhtasari wa matokeo ya utafiti, hitimisho la utafiti na mapendekezo ya mtafiti.

5.2 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti

Utafiti huu ulichunguza changamoto za utohoaji wa maneno ya Kiingereza katika lugha ya Kiswahili nchini Tanzania. Katika utafiti huu, mtafiti aliongozwa na lengo kuu la utafiti na malengo mahsuisi matatu ambayo ni; kubainisha mbinu za utohoaji wa maneno ya Kiingereza katika lugha ya Kiswahili, pili kuelezea athari za utohoaji wa maneno ya Kiingereza katika lugha ya Kiswahili, tatu ilikuwa ni kufafanua changamoto za utohoaji wa maneno ya Kiingereza katika lugha ya Kiswahili. Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kuwa utohoaji wa maneno ya Kiingereza kwenda katika lugha ya Kiswahili, hutumia mbinu mbalimbali kama vile; utohoaji wa moja kwa moja na mabadiliko ya matamshi, utohoaji wa moja kwa moja bila mabadiliko ambapo neno huchukuliwa kama jinsi lilivyo kimuundo na kimaana kutoka katika lugha changizi, udondoshwaji wa irabu kutoka katika lugha ya kiingereza, mbinu ya uchopekaji wa irabu hufanyika katikati ya neno au huweza kuwa mwishoni mwa neno na udondoshaji wa konsonanti katika konsonaanti kikundi.

Lengo la pili la utafiti huu ni kuonesha athari za utohoaji wa maneno ya Kiingereza katika lugha ya Kiswahili, ambapo matokeo ya utafiti huu yanaonesha athari za utohoaji wa maneno ya Kiingereza katika lugha ya Kiswahili kama ifuatavyo;

Ukuzaji wa msamiati wa lugha ya Kiswahili, athari hii ya ukuaji wa msamiati imeelezwa vizuri na watafitiwa 39 kati ya 43 sawa na 90% wameonesha kuwa, mbinu mbalimbali za utohoaji wa maneno ya Kiingereza katika lugha ya Kiswahili husababisha ukuaji wa maneno katika lugha pokezi, ambapo ni dhahiri kuwa kila lugha lazima itohoe maneno ili ijitosheleza katika mawasiliano yake, ambapo athari ya ukuaji wa msamiati wa lugha ya Kiswahili umeweza kujitokeza kutoka katika lugha ya Kiingereza kwenda katika lugha ya Kiswahili, umejidhirisha kutoka katika sekta ya afya, sekta ya elimu na pia katika sekta ya biashara, ambapo ongeziko la msamiati huo kwa namna moja ama nyengine husababisha pia ongeziko la watumiaji wengi wa lugha hiyo.

Pia zipo changamoto mbalimbali ambazo zimejitokeza kutoka katika lugha ya Kiingereza kwenda katika lugha ya Kiswahili, ambapo matokeo ya utafiti huu yanaonesha kuwa kuna changamoto za utohoaji wa maneno ya Kiingereza katika lugha ya Kiswahili kama vile ; mifuatano ya sauti isiyo katika muundo wa lugha ya Kiswahili, ambapo hupelekea kuwa na maneno yenye mifuatano ya herufi ambatano ambayo haipo katika matumizi ya lugha ya lugha Kiswahili.

Vile vile kuna ukiukwaji wa kanuni mkazo katika utamkwaji wa maneno ya lugha ya Kiswahili, ambapo neno hutoholewa kama lilivyo bila mabadiliko lakini kuna utofauti wa matokezi ya mkazo kutoka lugha changizi kwenda katika lugha pokezi.

Sambamba na hilo pia hudumaza lugha, miongoni mwa mbinu za utohoaji husababisha lugha kudumaa kwa kutohoa maneno kutoka lugha ya Kiingereza na kutoholewa kama yalivyo katika lugha ya Kiswahili, ambapo kwa namna moja ama nyengine

hudumaza lugha kwa kushindwa kupata maneno halisi yatakayotumika katika lugha ya Kiswahili.

Changamoto nyengine ni kasumba ya wazungumzaji wa lugha ya Kiingereza, maneno yanaweza kutoholewa si kwa kuwa hayapo katika lugha husika, bali ni kutoana na mtu kuwa na uwezo wa kuzungumza lugha zaidi ya moja, na hatimaye kusababisha lugha pokezi kuonekana kuwa duni.

Vile vile kuna upungufu wa mbinu za utohoaji. Data za utafiti zinaonesha kuwa kuna upungufu wa mbinu za utohoaji, kuna baadhi ya mbinu kama mbinu ya utohoaji wa moja kwa moja bila ya mabadiliko, mbinu hii haioneshi utofauti wa maneno yaliyotoholewa na badala yake imeweza kuhamisha maneno ya lugha ya changizi kwenda katika lugha ya Kiswahili kama yalivyo kimuundo, hivyo ipo haja ya kuwa na mbinu nyingi ili kuwe na urekebishaji wa maneno na yaoneshe kuna utofauti kati ya neno kutoka katika lugha changizi lililotoholewa kwenda katika lugha pokezi.

5.3 Hitimisho

Sura hii imezungumzia muhtasari wa utafiti kwa kuonyesha kuwa, utafiti huu umefanikiwa kutambua chanzo cha tatizo la changamoto za utohoaji wa maneno ya lugha ya Kiingereza katika lugha ya Kiswahili. Aidha katika utafiti huu tulibaini kuwa, ili lugha ikue ni lazima itohoe baadhi ya maneno kutoka katika lugha nyingine ili iweze kujitosheleza katika mawasiliano yake, kufanya hivyo ni kutokana na maendeleo makubwa ya sayansi na teknolojia, ambapo maneno mengi mapya hutokea, hivyo hakuna namna lugha iweze kutumia mbinu mbalimbali za utohozi wa maneno hayo.

5.4 Mapendekezo ya Utafiti

Kwa kuzingatia matokeo ya utafiti huu, mapendekezo mbalimbali yametolewa na mambo yafuatayo yamependekezwa nayo ni kama ifuatavyo;-

Kwanza, utafiti huu umeshughulika na changamoto za utohoaji wa maneno ya Kiingereza katika lugha Kiswahili, hivyo mtafiti anapendekeza kwamba, watafiti wengine wanaweza kufanya tafiti juu ya changamoto za utohoaji wa maneno ya lugha za Kiarabu, Kireno, na au Kijerumani katika lugha ya Kiswahili.

Pili mtafiti anapendekeza ipo haja ya watafiti wengine kuangalia njia za kutatua changamoto hizo za utohoaji wa maneno ya Kiingeeza katika lugha ya Kiswahili, ili kupunguza makosa madodgo madogo ambayo yanayojitokeza katika utohoaji wa maneno mbalimbali.

MAREJELEO

- Agyekum, K. (2006). "The Sociolinguistics of Akan Personal Names", *International Journal of Humanities and Social Science*, Vol.15(2): 206–235: University of Ghana.
- Arlotto, (1972). *Swahili Grammar*. Longman Green & Co. Ltd. London.
- Batibo, H.M. (2000). Foreign words as a problem in standardization/lexicography: English and African Loan words in isiXhosa" Anja Drame, Department of African Studies, university of Leipzig, Leipzig German, 231-2
- BAKIZA (2010). *Kamusi la Kiswahili Fasaha*, Nairobi: Oxford University Press.
- Best J.W and Khan J.V,(2006). *Research in Education*.(10th ed),New York:Pearson Education inc.
- Crystal, D. (1987). *The Cambridge Encyclopedia of Language*, 2nd edition. Cambridge: Cambridge University Press
- Enon, J. C. (1998). *Education Research, Statistics and Measurement*. Kampala: Makerere University Press. Griffen,
- Furlong na Lovelace 2000). *An Introduction to Language* (fourth ed). USA: Harcourt Brace Jovanovich College Publishers.
- Iribemwangi, P. I and Mukhwana, (2011:157). *Isimu jamii*. Nairobi focus publisher
- Karekezi, N. (2007). "Uundaji wa Istlahi za Kiswahili" Makala iliyowasilishwa katika kongamano la kimataifa la Idhaa za Kiswahili Duniani Tarehe 12-15 Oktoba lililoandaliwa na BAKITA.

Kenstowizs na Suchato (2006). Language planning and language reform in Kenya. Language Planning for Development in Africa. (UK. 37 – 54). Eldoret: Moi University Press.

Kombo D.K. and Tromp, D.L.A (2006), Proposal and Thesis writing: Introduction. Nairobi, Paulines Publications Africa.

Kothari (2009) Research Methodology; Methods. New Delhi New Age International Publishing LTD Techniques.

Kothari, C. R (2004). Research Methodology and Techniques. New Delh: New Age International (P).

Kress, C. S. (1998). Critical Praxis, Research. Breathing New life in to Research Methods for Teachers. United States of America: Springer.

Massamba D .P.B (2004) . Kiswahili Musoma: Mwanzo wa lahaja nyingine? Katika jarida la Taasisi ya uchunguzi wa Kiswahili. Dar es Salaam.

Massamba, D.P.B. (1977). A Comparative Study of Ruri, Jita and Kwaya Languages of Eastern Shores of Lake Nyanza (Victoria)“. University of Dar es Salaam. M.A Dissertation. Unpublisher.

Massamba, D.P.B (1989:62) “Development and modernization of Kiswahili Language in Tanzania” in F. Coulmas (ed) Language Adaptation. Cambridge, C.U.P, 60-78.

Massamba, D. P. (2010). *Isimu Jamii Sekondari na Vyuvo*, Dar-es-Salaam, TUKI.

Mbaabu, I. (2007). *Historia ya Usanifishaji wa Kiswahili*. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: TUKI.

Mbonankira, G. (2004). "The Accommodation of Kiswahili and English Words into Kinyarwanda". Unpublished Master's thesis, University of Nairobi, Nairobi, Kenya.

Mbunda, J. (2002). *New Horizons in Kiswahili: A synthesis in developments, research and literature*. Nairobi, Kenya Literaturebureau.

Ngonyani, D. (1989). *A Comparative Study of Kindendeule, Kingoni and Kimatengo*. Dar es Saalam: University of Dar es Saalam. M.A Dissertation. Unpublished.

Omary, C. and Richards, I. A. (1966), "Person Names in Social-cultural context". (Journal of the Institute of Swahili Research), Vol.No.2:40 sep, 1970, Dar-es-Salaam Chuo Kikuu Cha Dar-es-Salaam, Tanzania.

Owino, D. (2003). "Phonological nativization of dholuo loanwords" unpublished Master's thesis, university of Pretoria, Pretoria, South Africa.

Oxford Advanced Learner's Dictionary 7th edition (2005): Oxford University Press, India.

Sankoff G. Outcome of Language Contact pp 638-668. In *Hand Book of Sociolinguistics*. Trudgill, P. Chambers J. and Schilling N (ed) (2001). Oxford: BasilBlackwell.

Shariff Noor (1988:4). Loanwords and the Borrowing Language's Pre-Borrowing Phonology. Katika Christie Jnr (Mhr) Current Progress in Historical Linguistics. New York: North Holland Publishing Company.

Sigh K. (2007) Research Methodology; Methods, India, state SAGE publication
 Thomason, S. (1976). Contact induced language Changes: loan words and borrowing languages pre- pre borrowing phonology. In William Christie, ed Current Progress in historical Linguistics: Amsterdam: North Holland, 167-179.

Smith, J. L. (2006). Loan Phonology is not all Perception: Evidence from Japanese loan doublets. In T. J. Vance & K. A. Jones (Eds.) Japanese /Korean linguistics, Volume 14, 63-74. Stanford: CSLI.

Thomason, S. & Kaufman, T. (2001). Language Contact creolization and generic Linguistics. Barckley, Calfonia. University of Calfonia Press: 65-109, and 215-28.

TUKI (2013) Kamusi ya Isimu na Lugha, Dar-es-salaam: Education Publishers and Distributors.

TUKI (1990). Kamusi ya Isimu na Lugha, Dar-es-salaam: Education Publishers and Distributors.

Walliman, N. (1999). Research Methods: The Basics. London. Routledge Taylor and Francis Group.

Zawawi, S. (1979). Loanwords and their effect on the Classification of Swahili
Nominals: Leiden: E. J Brill., 73.

VIAMBATISHO

KIAMBATISHO 1: DODOSO

Mimi ni “Mtoro M. Bakari” mwanafunzi wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Ninafanya utafiti kuhusu “*Changamoto za Utohoaji wa Maneno ya Kiingereza Katika Kiswahili*”. Kwa heshima kubwa, ninakuomba muda wako ili uweze kujaza hojaji hii. Matokeo ya utafiti huu yatatumika kwa ajili ya kitaaluma tu na si vinginevyo.

SEHEMU YA A: MASWALI

Dodoso hili limewalenga wataalamu mbalimbali kutoka BAKITA na TATAKI

(Jibu maswali kwa kujaza sehemu zilizo wazi)

1. Je kuna uhusiano wowote wa kimsamiati au maneno ya lugha ya Kiswahili na Kiingereza?

(weka alama ya \surd kwenye mabano) Ndio () Hapana ()

2. Kama uhusiano upo utaje (kwenye swali la 1) na kama pia haupo toa maoni yako ni kwa vipi unafikri kuwahaupo.

.....

3. Eleza jinsi unavyoifahamu dhana ya lugha kutohoa maneno katika lugha nyingine?

.....
.....

4. Taja maneno walau 20 ya lugha ya Kiswahili yaliyotoholewa kutoka katika lugha ya Kiingereza. Taja maneno walau 20 ya lugha ya Kiswahili yaliyotoholewa kutoka katika lugha ya Kiingereza.

(a) (b) (c)

(d) (e)

5. Taja njia ambazo hutumiwa na Mtafiti wa lugha ya Kiswahili wanapotohoa maneno kutoka katika lugha ya kiingereza.

(a).....(b).....(c).....

6. Taja athari za lugha ya Kiswahili za kutohoa maneno kutoka katika lugha ya Kiingereza.

(a).....(b).....(c).....

(d).....(e).....

7. Changamoto zipi zinazojitokeza wakati wa kutohoa maneno ya Kiingereza kwenda katika lugha yaKiswahili?.

(a).....

.....
.....
.....

(b).....

.....

.....

(c).....

.....

.....

.....

(d).....

.....

.....

(e).....

Ahsante sana kwa kujibu hojaji hili

(Mtafiti)

Mtoro M. Bakari

KIAMBATISHO

BARUA YA KUKUSANYA DATA KUTOKA OUT

THE OPEN UNIVERSITY OF TANZANIA

DIRECTORATE OF POSTGRADUATE STUDIES

P.O. Box 23409
Dar es Salaam, Tanzania
<http://www.openuniversity.ac.tz>



Tel: 255-22-2668992/2668445
ext.2101
Fax: 255-22-2668759
E-mail: dpgs@out.ac.tz

Our Ref: PG201703073

University of Dar es salaam,
P o Box 35091,
D ar es salaam.

24th June 2019

RE: RESEARCH CLEARANCE

The Open University of Tanzania was established by an Act of Parliament No. 17 of 1992, which became operational on the 1st March 1993 by public notice No. 55 in the official Gazette. The Act was however replaced by the Open University of Tanzania Charter of 2005, which became operational on 1st January 2007. In line with the Charter, the Open University mission is to generate and apply knowledge through research.

To facilitate and to simplify research process therefore, the act empowers the Vice Chancellor of the Open University of Tanzania to issue research clearance, on behalf of the Government of Tanzania and Tanzania Commission for Science and Technology, to both its staff and students who are doing research in Tanzania. With this brief background, the purpose of this letter is to introduce to you **Mr. MTORO, Bakari M. Reg No: PG201703073** pursuing **Master of Arts in Kiswahili (MA- Kiswahili)**. We here by grant this clearance to conduct a research titled **"Changamoto za Utohoaji wa Maneno ya Kiswahili."** He will collect his data at Kinondoni District in Dar es salaam region from 19th June 2019 to 17th September 2019.

In case you need any further information, kindly do not hesitate to contact the Deputy Vice Chancellor (Academic) of the Open University of Tanzania, P.O. Box 23409, Dar es Salaam. Tel: 022-2-2668820. We lastly thank you in advance for your assumed cooperation and facilitation of this research academic activity.

Yours Sincerely,

Prof. Hossea Rwegoshora
For: VICE CHANCELLOR
THE OPEN UNIVERSITY OF TANZANIA